# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00089 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 20 - 26, 2024 |


## Morocco aipeleka Stars Morocco



Uk. 24



**RIPOTI:** Wanaume wanakufa kwa wingi na Ukimwi kuliko wanawake Uk. 2

## Wachezaji hawa ni uti wa mgongo Simba

Uk. 23



KUELEKEO UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA:

## Tuwasikilize wagombea, tuchague kwa usahihi



Uk. 23

# Rais Dk. Samia anguruma G20


■ Ayataka mataifa tajiri kushiriki kutokomeza umaskini Afrika



UZINDUZI KAMPENI UCHAGUZI S/MITAA:

## CCM yamwaga viongozi na makada nchi nzima

● Atoa nishani kwa Wachungaji



Uk. 4

## ... aongeza saa 24 uokoaji



Uk. 4




### JANGA LA KARIKOO:

# Wawili matatani tuhuma za 'kuvuta' michango kinyemela

**Na Mwandishi Wetu**

WATU wawili wametiwa mbaroni kwa tuhuma za kushughulikia majanga yenye sura ya kitaifa kwa kuanza kukusanya fedha kwa kutumia akaunti zao binafsi, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria na Kanuni zinazoshughulikia majanga.

Watuhumiwa hao wanaoshikiliwa na Jeshi la Polisi ni Diva Gissele Malinzi (36) mkazi wa Mikocheni Dar es Salaam maarufu kama Diva na Jenifer Jovin Bilikwija maarufu kama Niffer (25), mkazi wa Salasala, Kinondoni ambaye alikamatwa akiwa Dodoma na kurejeshwa Dar es Salaam.

Taarifa ya Jeshi la Polisi ilieleza jana kuwa watuhumiwa hao walikamatwa na wanahojiwa kwa kina.

Sambamba na hilo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam,



litashirikiana na mamlaka nyingine za kisheria kuona hatua zaidi zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa hao.

Aidha, Jeshi la Polisi limetoa tahadhari na kwamba halitasita kuchukua hatua za kisheria kwa mtu au watu ambao yanapotokea matatizo au majanga, huona ni fursa ya kujinufaisha.

Jengo la ghorofa eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam, liliporomoka Novemba 16, mwaka huu.

Hata hivyo, wakati jitihada mbalimbali zikifanywa na serikali na sekta binafsi jinsi ya kuwaokoa waahirika wa tukio hilo, watu wasio na mamlaka yoyote ya kisheria ya kushughulikia majanga yenye sura ya kitaifa, kuanza kukusanya fedha kwa kutumia akaunti zao binafsi, suala ambalo ni kinyume cha Sheria na Kanuni zinazoshughulikia majanga.

# Anayekumbatia watoto njiti aula tena

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupata ajira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kukumbatia watoto njiti katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana,

Taasisi ya Doris Mollel, imemkabidhi Mariam Mwakabungu (26) nyumba ya makazi yenye thamani ya Sh. milioni 45.

Makabidhiano hayo yalifanyika Chanika-Zavara jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Watoto Njiti Duniani.

Mariam alifikishwa sehemu ambayo nyumba yake imejengwa akiwa amefungwa kitambaa usoni na kuongoza na mumewe Christopher Nyoni (30) kama tukio la kumshtukiza.

Alikabidhibiwa nyumba na taasisi hiyo kama ishara ya kutambua mchango wake.

Nyumba hiyo aliyozawadiwa na msamaria mwema ambaye hakutaka jina lake litajwe, imejengwa na Taasisi ya Doris Mollel Foundation kwa kushirikiana na wadau wengine waliochangia baadhi ya vifaa.

Julai 20, mwaka jana, Serikali kupitia Wizara ya Afya, ilitoa ajira ya mkataba kwa Mariam, ikiwa ni siku moja tangu Rais Dk. Samia kutuma salamu za pongezi zilizoambatana na Shilingi milioni mbili.

Mariam alimshukuru Mungu, Taasisi ya Doris Mollel Foundation, Wizara ya Afya na Uongozi wa Hospitali ya Amana.




Taasisi ya Doris Mollel, imemkabidhi Mariam Mwakabungu (26) nyumba ya makazi yenye thamani ya Sh. milioni 45.

# Tuzo ya Mwalimu Nyerere kuchochea uandishi, usomaji vitabu

**Na Mwandishi Wetu**

TUZO ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu inatarajiwa kuendelea kuchochea uandishi wa vitabu na usomaji nchini, huku ikichangia kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili na hazina ya vitabu katika maktaba.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo hivi karibuni wakati wa hafla ya Uzinduzi wa Ugawaji wa Vitabu Vilivyoshinda tuzo hiyo kwa mwaka 2022/23 na kimoja cha mwaka 2023/24.

Akizungumza katika hafla hiyo, Profes Mkenda alisema tuzo hizo zinalenga kuhamasisha Watanzania kuandika vitabu bora vinavyokidhi maadili na kusaidia matumizi katika shule.

"Tuzo hii itaendelea kuwahamasisha waandishi wengi kuandika vitabu vizuri na vyenye maadili, ambavyo vitatumika shuleni kwa watoto wetu. Pia, itawafanya Watanzania wengi kupenda kusoma vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili," alisema.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kuipa nguvu Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ili kuhakikisha tuzo hii inafanyika kila mwaka kwa kushirikisha watu wengi zaidi.

Alitoa wito kwa waandishi wenye vipaji kuwasilisha miswada yao kwa ajili ya kushindania tuzo ya mwaka 2024/25.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Tuzo hiyo, Profesa Penina Mlama, aliwahimiza Watanzania kujitokeza kwa wingi kuwasilisha miswada yao kwa ajili ya mashindano ya tuzo zijazo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdulla Said, alisema vitabu vilivyoshinda vitagawiwa shuleni ili wanafunzi wapate maarifa kupitia maandiko hayo bunifu.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la TET, Prof. Maulid Mwatawala, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za TET na kueleza kwamba maandalizi ya vitabu vya mtaala mpya yamekamilika kwa mafanikio.

Mkurugenzi Mkuu wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema vitabu vilivyoandikwa na washindi wa tuzo hiyo vitaanza kusambazwa shuleni kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi kujifunza kwa urahisi.

Vitabu vilivyozinduliwa ni Zawadi (Hadithi za Watoto) kilichoandikwa na Blandina Isabella Lucas, Gereza la Kifo (Riwaya) cha Hamisi Kibari, na Mtale wa Ngariba (Ushairi) kilichoandikwa na Amri Abdallah, ambavyo vimechapishwa kwa udhamini wa Serikali na Benki ya Duni




# Majaliwa ataja malengo wachimbaji wa kati 2030

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema malengo ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, wachimbaji wadogo wanakuwa wachimbaji wa kati ili kuongeza mchango wao katika uchumi wa taifa.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini unaobeba kauli mbiu "Uongezaji Thamani ya Madini kwa Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii."

Aidha aliiagiza Wizara ya Madini kusimamia vyama vya wachimbaji wadogo wa madini ili kuhakikisha wanazingatia sera na sheria zilizopo za uchimbaji, na hivyo kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema sekta ya madini imeendelea kukua kwa kasi na serikali inajipanga kuboresha zaidi mazingira ya wachimbaji wadogo.

Alisema malengo ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, wachimbaji wadogo wanakuwa wachimbaji wa kati ili kuongeza mchango wao katika uchumi wa taifa.

"Niwaelekeze Wizara ya Madini muendelee kusimamia vyama vya wachimbaji madini. Hatua hii itasaidia kukuza na kuimarisha soko la madini nchini na kuvutia wawekezaji wengi zaidi," alisema.

Pamoja na hayo, Waziri Mkuu aliwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa za uwekezaji katika sekta ya madini, akisisitiza kuwa Tanzania imejipanga vyema kimkakati na ina maeneo mengi yanayofaa kwa uwekezaji.

Akijibu ombi lililotolewa na Chama cha Wachimbaji Wadogo wa Madini (FEMATA) kuhusu kupatiwa leseni, Waziri Mkuu alisema serikali tayari imefanya mapitio ya sera na inaendelea na mchakato wa kutoa leseni hizo kwa wachimbaji wadogo kutumia maeneo yaliyorejeshwa serikalini.

Aidha, aliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo yote ya uchimbaji, akibainisha kuwa Tanzania sasa ina uwezo wa kuzalisha umeme wa kutosha.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa

**KWA UFUPI:**

# Tz na Uturuki kushirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Uturuki, zimekubaliana kushirikiana kukuza sekta ya Maliasili na Utalii lengo likiwa ni kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchi hizo mbili.

Hayo yalielezwa wakati wa kikao kati ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana na Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Dk. Mehmet Gulluoglu, kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) jijini Dar es Salaam jana.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana

# Rais Dk. Samia anguruma G20

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ameandika historia kuwa kiongozi wa kwanza mwanamke kutoka Afrika, kushiriki na kuzungumza kwenye mkutano wa mataifa 20 tajiri duniani (G20).

Rais Dk.Samia ameshiriki mkutano wa siku mbili wa G20 uliofanyika jijini Rio de Janeiro, Brazil Novemba 18 na 19, mwaka huu na kupata nafasi ya kuwahutubia viongozi wa mataifa makubwa kama Marekani, Uingereza na China.

Akihutubia katika mkutano huo, Rais Dk. Samia ametoa wito kwa mataifa tajiri duniani kutambua na kuzitumia fursa zilizopo barani Afrika na kushiriki kutokomeza umasikini uliokithiri.

Miongoni mwa viongozi walioisikiliza kwa makini hotuba ya Rais Samia ni Rais wa Marekani Joe Biden, Rais wa China Xi Jinping na Waziri Mkuu wa Uingereza Keir Starmer.

Dk. Samia aliyeshiriki mkutano huo kwa mwaliko wa Rais Lula da Silva wa Brazil, alisema wakati dunia ikiwa na utajiri mkubwa, Afrika inakabiliana na umasikini uliokithiri, njaa, maradhi, utapiamlo na uzalishaji duni.




## ... aongeza saa 24 uokoaji

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amemuelekeza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kuongeza saa 24 za uokoaji katika jengo lililoporomoka eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninatambua utaratibu wa uokoaji una muda maalum wa saa 72 mpaka kusitisha zoezi hilo.

"Binafsi nina matumaini kuwa Mwenyezi Mungu anaweza akatenda miujiza yake na kuwanusuru ndugu zetu wengine ambao bado wamenasa kwenye jengo hilo.

"Ninakupa maelekezo ya kutositisha zoezi la uokoaji na kuongeza muda wa saa 24 zaidi ili kuwapambania ndugu zetu ambao tunaamini bado wako hai," alisema jana kupitia akaunti ya mtandao wake rasmi wa Instagram.

Taarifa hiyo ilitolewa kufuatia mazungumzo yake na Waziri Mkuu Majaliwa kwa njia ya simu kuhusiana na zoezi la uokoaji.

Aidha, Rais Dk. Samia alisema anatambua na kuthamini mchango wa wananchi wote wanaopambana kuokoa maisha ya walioangukiwa na jengo hilo.

"Kwa vikosi vyetu vyote na wananchi wote wanaopambana kuokoa maisha ya ndugu zetu katika zoezi hilo, ninaomba ufikishe salamu zangu na uwaeleze kuwa natambua na ninawathamini sana," alisema na kuongeza:

"Wameonyesha utu, uzalendo mkubwa na uchapakazi wa hali ya juu sana. Hivyo, nawatia moyo na kuwapa nguvu ya kuendelea kuwapambania ndugu zetu kwani ninyi ni mashujaa wa taifa letu."

Kwa upande mwingine, Rais Dk. Samia amewasihi wananchi, ndugu na jamaa, kuendelea kuwa na subira na kama Taifa kuendelea kuwaombea ndugu na wapiganaji ili kufanikisha zoezi hilo kwa mafanikio makubwa.

## CCM yamwaga viongozi na makada nchi nzima

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, leo anatarajiwa kuzindua kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za CCM Mkoa wa Mwanza.

Balozi Dk. Nchimbi ambaye pia ni Mlezi wa CCM Mkoa was Mwanza, atawaongoza viongozi na makada wa Chama waliotumwa maeneo mbalimbali nchini kwa kazi hiyo.

Atazindua kampeni hizo katika mkutano wa hadhara utakaofanyika Uwanja wa Furahisha, Nyamagana, jijini Mwanza.

Wajumbe wa Kamati Kuu ya CCM ambao ni walezi wa mikoa mingine na Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), wamepewa jukumu la kuzindua kampeni hizo katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara leo hii.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM (Bara), John Mongella, atazindua kampeni Mkoa wa Mbeya, huku Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Mohamed Said Mohamed Dimwa, akizindua kampeni Mkoa wa Katavi.

Baadhi ya viongozi wengine wa CCM waliopangiwa kuzindua kampeni mikoa yao kwenye mabano ni Makamu wa Rais Dk. Isidory Mpango (Dodoma) na Katibu wa NEC - Oganaizesheni Issa Haji Usi Gavu (Geita).

Wengine ni Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo , Amos Makalla (Dar es Salaam), Katibu wa NEC - Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Rabia Himid Abdalla (Kilimanjaro,) na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (Kigoma).

Wengine ni Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda () Mtwara), Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar Mohammed Abdulla Suleiman (Tanga) na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zuber Ali Maulidi (Singida.)

Wengine ni Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda (Arusha), Halima Mamuya (Njombe),

Nasir Ally Juma (Tabora), Mohamed Aboud Mohamed (Iringa), Mwenyekiti wa UVCCM Taifa, Mohamed Ali Kawaida (Morogoro), Mwenyekiti wa Wazazi Taifa, Fadhili Maganya (Simiyu) na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto (Mara).

Mkakati huu wa kuzindua kampeni kwa mtindo wa ushirikiano wa karibu kati ya viongozi wakuu na wanachama, unaonesha jinsi CCM inavyothamini uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Pia, unadhihirisha dhamira ya kupata ushindi mkubwa dhidi ya vyama vya upinzani, ambavyo hadi sasa vimeshindwa kusimamisha wagombea wa kutosha kushindana kikamilifu.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi

# Maafisa madini wakazi mikoa wapewa neno

Na Mwandishi Wetu

MAAFISA Madini Wakazi wa mikoa wametakiwa kuongeza usimamizi wa mazingira kwenye shughuli za utafiti, uchimbaji na uchenjuaji wa madini ili kuepuka ajali na kusababisha vifo.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti mpya wa Tume ya Madini, Janet Lekashingo, katika kikao chake na menejimenti ya Tume ya Madini ikihusisha Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini, Mhandisi Ramadhani Lwamo, Wakurugenzi, Mameneja na Maafisa Madini Wakazi wa Mikoa kilichofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Lengo la kikao hicho lilikuwa ni kuweka mikakati ya kuimarisha sekta ya madini hasa kwenye eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2024/2025.

Sambamba na kupongeza kwa kasi ya ukusanyaji wa maduhuli inayofanywa na Maafisa Madini Wakazi wa Mikoa, alisema ni vyema suala la usimamizi wa mazingira kwenye shughuli za madini likazingatiwa ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji wa madini zinafanyika pasipo kuathiri mazingira.

Aidha, aliwataka maafisa hao kuendelea kutatua changamoto nyingine katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na migogoro kati ya wachimbaji wa madini na jamii inayowazunguka, kiteknolojia na kuongeza ubunifu kwenye utendaji kazi.

Kadhalika, aliwataka kuendelea kushirikiana kama timu moja na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya madini.

Naye Mwenyekiti wa Maafisa Madini Wakazi wa Mikoa ambaye ni Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Simiyu, Mayigi Makolobela, akizungumza kwa niaba ya maafisa hao, alipongeza uteuzi wa Mwenyekiti mpya na kuongeza kuwa siri ya uteuzi wake ni kutokana na historia nzuri ya utendaji kwenye sekta ya madini.

Aidha, amewataka maafisa hao kuendelea kutatua changamoto nyingine katika sekta ya madini ikiwa ni pamoja na migogoro kati ya wachimbaji wa madini na jamii inayowazunguka, kiteknolojia na kuongeza ubunifu kwenye utendaji kazi.

Vilvile, aliwataka kuendelea kushirikiana kama timu moja na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta ya madini.






# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

### Trafiki wanapogeuka roboti

Ni kweli, taratibu na sheria zinataka magari yasiyosajiliwa kama ya kubeba abiria yasibebe abiria. Lakini kuna nyakati za jioni au asubuhi katika Jiji kama la Dar es Salaam usafiri unakuwa mgumu sana, lakini gari ndogo zikisimama kwenye vituo vya daladala kusanya na kusaidia wananchi usafiri zinakamatwa kwa kuwa hazijasajiliwa kwa ajili hiyo.

Sheria au kanuni hii inapaswa kuangaliwa upya kwa sababu haina tija na inaongeza ugumu wa maisha bila sababu. Kibaya zaidi askari wa usalama barabani wanaitumia hii kuwapiga bao wenye kutaka kusaidia abiria na kuvuna pesa wao.

Yaani wakati wanaona hali ya usafiri ilivyo mbaya bado wanazuia magari madogo kusaidia abiria kuwahi kazini au majumbani. Huku ni kufanya kazi mithili ya roboti.




MAONI YA MHARIRI

## Magizo ya Rais Samia yatekelezwe barabara

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameeleza kupokea maelekezo ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan ya Serikali kuunda Tume ya watu 19 itakayopitia maghorofa yote katika eneo la kibiashara la Kariakoo ili kutambua ubora wa kila jengo.

Hatua hiyo imetokana na kuanguka kwa ghorofa katika eneo hilo la Kariakoo Novemba 15, na kusababisha vifo vya watu 16 vilivyokuwa vimethibitika hadi tunakwenda mitamboni huku wengine zaidi ya 80 wakiokolewa kwenye vifusi.

Akizungumza juzi Novemba 18, katika tukio la kuiaga miili ya watu waliopoteza maisha katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Kariakoo Dar es Salaam, Majaliwa alitabaisha kuwa, Tume hiyo itasaidia kutambua na kuishauri serikali nini ifanye baada ya uchunguzi huo.

Alisema Soko la Kariakoo kwa sasa linategemewa na nchi zote zinazotuzunguka hapa jirani na kwamba tunayo sababu ya kuliimarisha lakini pia kutambua ubora wa majengo yaliyopo ili wajasiriamali waendelee kufanya biashara zao kwa miongozo mipya itakayotolewa na serikali baada ya Tume hiyo kuchunguza na kutoa ushauri kwa serikali.

Majaliwa alisema Tume hiyo itaongozwa na Mwenyekiti wake, Brigedia Jenerali Hosea Ndagala ambaye ni Mkuu wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu na Katibu wake atakuwa Mhandishi Melecky Mwano kutoka Bodi ya Usajili ya Wakandarasi.

Tunashukuru kwa uamuzi huu kwani ujenzi unaondelea eneo la Kariakoo kwa kweli unaacha maswali mengi kwani tunashuhudia maghorofa yakiendelea kuibuka kila kukicha kama uyoga.

Kuvunjwa na kuibuka kwa mghorofa si jambo baya lakini suala ni kama ujenzi wake unafuata utaratibu na kuzingatia kanuni zinazotakiwa kwani kuna hofu kwamba mengi yanajengwa kwa njia ya kulipua.

Tumesikia habari ya wafanyabiashara kununua maghorofa ama nyumba za zamani na kuzivunja, kisha kujenga hayo maghorofa kwa kasi ya kimbunga.

Wapo waliodai kushuhudia jengo la ghorofa nne hadi tano likijengwa ndani ya mwezi mmoja kitu ambacho wengi wana wasiwasi na hilo. Lakini ukiacha hayo yanayoibuka kama uyoga, yapo makongwe ambayo yamechoka, lakini badala ya kuvunjwa, yanaongezewa majukumu!

Hivyo tunategeemea agizo la Rais, Dk. Samia litafanyiwa kazi barabara kwa maghorofa na majengo haya ya Kariakoo kufanyiwa tathimini ili viwango vya ubora wake vibainike. Na tunaamini haitaishia kubaini tu bali kuchukua hatua ya kuyavunja.

La sivyo huko mbele tutakuja kulia zaidi kuliko tunavyolia sasa!

Wasiliana nasi

Mhariri Mkuu: +255713263775 / +255748115000
Mhariri wa Habari: +255768411003
Mhariri Michezo: +255784122020
Meneja Masoko/Biashara: + 255718480406 / + 255733768825
S. L. P: 15110, Dar es Salaam
Makao Makuu Mtaa: Barabara ya Morogoro
Jengo la: Aura Mall
Chumba Cha Habari: +255 (0)222151532
Email: uelekeohabari@gmail.com

Na Hamisi Kibari

JICHO LANGU

## Ni kweli, tuwaenzi waandishi wetu wa fasihi

**Na Mwandishi Wetu**

JUZI Jumatatu, Novemba 18, kulikuwa na hafla ya Uzinduzi wa Ugawaji Vitabu Vilivyoshinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa mwaka 2022/2023 na kimoja 2023/2024.

Katika hafla hiyo, vitabu vilivyoshinda Tuzo za Mwalimu Nyerere na kuzinduliwa tayari kwa kugawiwa baada ya kuchapishwa ni vya Blandina Isabella Lucas aliyeshinda hadithi za watoto kupitia kitabu chake za Zawadi, Hamisi Kibari aliyeshinda Riwaya kupitia muswada wake wa Gereza la Kifo na Amri Abdallah aliyeshinda ushairi kupitia muswada wake wa Mtale wa Ngariba.

Katika hafla hiyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisisitiza umuhimu wa kuwaenzi waandishi nguli wa vitabu wa Tanzania ambao wameacha alama katika uandishi wa vitabu na kukuza fasihi ya Kiswahili. Aliona kwamba kuna haja ya 'kuwapa maua yao' wakiwa bado hai.

Alisema ni muhimu kutoa heshima kwa waandishi kama Shafi Adam Shafi, Prof. Penina Mlama, Prof. Amandina Lihamba, Prof. Saida Yahya-Othman na wengine mfano wa hao kwa mchango wao mkubwa katika fasihi ya Kiswahili. Magwiji hao wa vitabu wameshiriki hafla hiyo.

Prof. Mkenda alielezea masikitiko yake kwa kutokuwa na alama za kudumu kama majina ya shule au barabara zilizotolewa kwa heshima ya waandishi hawa nguli, akitolea mfano wa Sierra Leone, ambako kuna shule imepewa jina la Penina Mlama.

Alisisitiza pia umuhimu wa kutafsiri kwa Kiswahili kazi za mwandishi wa vitabu Mtanzania, Abdulrazak Gurnah, mshindi wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi, kwani kazi zake tayari zimeshafsiriwa kwa lugha zingine ikiwemo Kichina.

Kwa ninamuunga mkono Waziri Mkenda, kwanza kuanzisha tuzo hiyo, lakini pia kwa hicho alichokiona kwamba ipo haja ya kuwaenzi zaidi watunzi wa vitabu wa Tanzania ambao wameacha alama katika uandishi wao waandishi hata waandishi vijana ili kuhamasisha uandishi na usomaji wa vitabu.

Mbali na hao aliowataja, nchi hii pia imekuwa na waandishi waliofanya vizuri kama Faraji Katalambula, Eddie Ganzel, Ben Mtobwa, Hammie Rajab, Jumaa Mkabarah, John Simamwene, Kajubi Mkajanga, Hussein Tuwa na wengineo.

Kadri tutakavyoweza ni vyema kuwaenzi waandishi wetu wa fasihi.

**Katika hafla hiyo, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisisitiza umuhimu wa kuwaenzi waandishi nguli wa vitabu wa Tanzania ambao wameacha alama katika uandishi wa vitabu na kukuza fasihi ya Kiswahili. Aliona kwamba kuna haja ya 'kuwapa maua yao' wakiwa bado hai.**

# Zifahamu dalili 10 za ugonjwa wa kisukari



MKUNUNGU Koswako (siyo jina lake halisi), hakuelewa kwamba alikuwa na ugonjwa wa kisukari kwa muda mrefu.

Koswako hakujua kwamba sababu za kujihisi kiu, uchovu na mwili kuishiwa nguvu, huenda ni baadhi ya dalili za maradhi hayo.

‘’Nilikwenda kwa daktari na kumueleza baada ya kujisikia vibaya kwa muda mrefu. Alinifanyia vipimo vya kisukari na magonjwa mengine. Ni pale ndipo niligundulika kuwa nina ugonjwa wa kisukari kwa muda mrefu,’’ anasema Koswako.

Tangu hapo, Koswako alianza matibabu katika hospitali maalum ya ugonjwa wa kisukari.

Si yeye pekee, kwa mujibu wa wataalamu wa kisukari, zaidi ya asilimia 50 ya watu wenye maradhi ya kisukari, hawafahamu kuwa wana ugonjwa huo.

Koswako aligundulika kuwa na ugonjwa huo alipokuwa akipimwa maradhi mengine.

Wataalamu wanasema kutokana na hali hiyo, ndiyo maana ni muhimu mno kutoa hamasa kwa jamii kuhusu ugonjwa wa kisukari.

Utafiti mmoja wa Taasisi ya Mafunzo ya Idadi ya Watu (NIPORT) unaonyesha kuwa katika jumla ya wagonjwa wa kisukari milioni 10, miongoni mwao ni wenye umri wa miaka 18 hadi 34 ambao ni 200,600 na idadi ya watu zaidi ya miaka 35 ni 800,400.



Wataalamu wanasema kwamba ikiwa ugonjwa wa kisukari haujatambuliwa au haujatibiwa kwa muda mrefu, figo, ini na macho huharibika.

Pamoja na hayo, ngozi ya mwili huharibika, nywele hudondoka. Sehemu nyingine za mwili, pia zinaweza kuathirika.

“Wale wanaofanya shughuli nyingi, kama vile kutembea angalau hatua 10,000 kila siku, hata kama ana kisukari, inawezekana kudhibiti. Hata hivyo, ni watu wachache mno wanaofanya hivyo.

Inashauriwa na wataalamu kwamba yeyote aliye na kisukari, lazima afanye mabadiliko ya mtindo wa maisha.

Inaendelea uk. 8

# Zifahamu dalili 10 za ugonjwa wa kisukari

>>>Inatoka Uk. 7

Wataalamu wanasema kwamba asilimia 75 ya ugonjwa wa kisukari cha aina ya 2, inaweza kuzuiwa ikiwa mgonjwa atakuwa mwangalifu mapema, kufanya mazoezi na kudhibiti lishe na mtindo wake wa maisha.

Lakini mara tu anapogundulika kuwa na kisukari, hakuna namna ya kuondoa ugonjwa huu, hivyo ni muhimu sana kuchukua hatua mara baada ya kuona dalili hizi:

- Kukojoa mara kwa mara na kiu
- Kuhisi udhaifu na kizunguzungu
- Kuongezeka kwa hamu ya kula
- Ikiwa hutakula na kunywa kwa wakati, sukari ya kwenye damu hupungua
- Kuongezeka kwa hamu ya pipi
- Kupoteza uzito mwingi bila sababu
- Jeraha au kukatwa kwenye mwili, huchukua muda mrefu kupona
- Ngozi kavu inayowaka na kuwasha
- Kuwashwa mwilini
- Macho kuanza kupoteza uoni



## NI NANI ALIYE KATIKA HATARI KUBWA ZAIDI?

Wataalamu wanasema kwamba wale ambao wazazi wao, ndugu au jamaa wa karibu, wana kisukari wako kwenye hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo.

Mbali na hilo, wale ambao hawana utamaduni wa kutembea mara kwa mara au kufanya mazoezi ya mwili, au wasio na mtindo ufaao wa maisha, wana hatari ya kuathiriwa na ugonjwa huu.

Kwa kuongezea, wanawake wanaweza kupata ugonjwa wa sukari wakati wa ujauzito.

Watu wenye magonjwa ya moyo, cholesterol kubwa ya damu, shinikizo la damu, pia wako katika hatari ya kupata ugonjwa huu.

Watoto walio na uzito mkubwa, wazazi, ndugu, babu au jamaa wa karibu wenye ugonjwa wa kisukari, ambao mama yao alikuwa na kisukari wakati wa ujauzito, wako katika hatari ya kupata kisukari.

## HATUA ZA KUZINGATIA

Wale ambao wako katika hatari, lazima wapimwe ugonjwa wa kisukari mara moja kwa mwaka.

## SIYO LAZIMA KILA WAKATI KWENDA HOSPITALINI.

Vipimo vya haraka vya kisukari sasa vinapatikana katika maduka mengi ya dawa kwa gharama nafuu.

Ikiwa utagundulika kuwa na ugonjwa wa kisukari, ni lazima kupata ushauri wa daktari.

Watoto ambao jamaa zao wa karibu wana historia ya ugonjwa wa kisukari wanapaswa pia kuchunguzwa angalau mara moja kwa mwaka.

Kisukari kinapogunduliwa mapema, ndivyo inavyokuwa vema kwa mgonjwa kwa kuwa ataanza matibabu ya ugonjwa huo haraka, mtindo wake wa maisha pia utadhibitiwa, wanaeleza wataalamu

BBC.

> **WATU wenye magonjwa ya moyo, cholesterol kubwa ya damu, shinikizo la damu, pia wako katika hatari ya kupata ugonjwa huu.**



*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Nov. 20-26, 2024






# Rais Dk. Samia ametuheshimisha kualikwa G 20

*Jarida hili haliuzwi*

UK. 12 & 13



UK. 7

## Zifahamu dalili 10 za ugonjwa wa kisukari

## Chadema, jahazi linalokwenda mrama



UK. 11

# Chadema, jahazi linalokwenda mrama




**Na Na Hamid Yassin**

HIVI karibuni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kilijitokeza hadharani kukanusha vikali tuhuma zinazohusishwa nacho, hasa kuhusu madai ya rushwa na ufisadi yanayoelekezwa kwa baadhi ya viongozi wake na yanayodaiwa kujitokeza ndani ya chama hususan katika chaguzi za ndani.

Taarifa hii ilitolewa siku ya Alhamisi Novemba 14, 2024 na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, ambapo alisisitiza kwamba, Chadema iko mstari wa mbele katika kupambana na vitendo vya ufisadi na rushwa.

"Tuhuma za Chadema kuwa na fedha chafu au rushwa ndani ya chama au katika chaguzi za chama. Tuhuma hizi zimekuwepo maeneo kadhaa, baadhi zimekosa vielelezo vya ushahidi wa kisheria na maeneo mengine bado uchunguzi wa ndani unaendelea," alieleza Mrema katika taarifa hiyo.

Mrema alisisitiza kuwa, Chadema haijawahi kupokea wala kujadili madai ya rushwa, na kwamba kama kuna ushahidi wowote wa tuhuma hizo, unapaswa kuwasilishwa haraka kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu dhidi ya wahusika.

"Chadema imekuwa mstari wa mbele kupambana na ufisadi, ubadhirifu na rushwa miaka yake yote. Kama chama kikiletewa ushahidi au vielelezo vya tuhuma hizo kutoka kwa mtu yeyote tutafanyia kazi haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa Katiba, Kanuni na Mwongozo wa Chama dhidi ya Rushwa wa Mwaka 2012," ameeleza Mrema.

## MALALAMIKO YA UFISADI YASEMWA NA VIONGOZI

Taarifa hii ya Chadema inajiri baada ya kuwa na malalamiko na taarifa za hapa na pale ambazo zimekuwa zikitolewa na wafuatiliaji wa siasa nchini Tanzania, wanachama wa chama hicho na viongozi wake wakubwa akiwamo Makamu Mwenyekiti wake Tanzania bara, Tundu Lissu.

Mjadala umebaki katika vinywa vya wengi juu ya athari ya shutuma hizo kwa chama hicho hasa wakati huu ambapo kinaelekea kushiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji, na Vitongoji Novemba 27, 2024.

Baada ya mara kadhaa kujitokeza hadharani, Lissu aliibuka tena hivi karibuni na kudai kuwa, Chadema kina fedha chafu inazozitumia kwenye chaguzi zake za ndani, lakini imeshindwa kusimamisha wagombea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwenye sehemu kubwa ya nchi.

Lissu alitangaza rasmi kuwa, chama hicho hakina ubavu wa kusimamisha wagombea katika majimbo yote ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika tarehe 27 mwezi huu.

Lissu aliyasema hayo katika mahojiano yake na kituo kimoja cha televisheni na kufafanua kuwa, hiyo inatokana na changamoto ya ukata unao vikabili vyama vingi vya upinzani.

Makamu Mwenyekiti huyo wa Chadema alisema kuna majimbo yapatayo 380,000 ya uchaguzi nchi nzima, hivyo kupata wagombea wote wa nafasi hizo si changamoto kwa wapinzani pekee bali hata kwa chama tawala CCM.

Lakini hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, wakati akitangaza kuwa kati ya rufaa 16,309 zilizowasilishwa na wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, rufaa 5,589 zimekubaliwa, alisema CCM imefanikiwa kusimamisha wagombea nchi nzima.

Waziri alisema kuwa vyama 18 vya siasa vimefanikiwa kuweka wagombea katika nafasi 30,977 kati ya nafasi 80,430 zinazogombewa, sawa na asilimia 38.51.

Lissu yeye alikaririwa akisema: "Kila Kijiji wanachanguliwa watu 25, kila mtaa wanachaguliwa watu 9, kuna vijiji 14,000 na mitaa ipo zaidi ya 6000 nchi nzima, ni ngumu kwa Chama kama Chadema kupata wagombea 380,000 ni kazi ngumu, hasa ukizingatia kuna changamoto fedha, changamoto za kupata wagombea, changamoto vifaa. Huwezi kushiriki uchaguzi kikamilifu kama huna wagombea mwafaka, huna vifaa vya kutosha vya kufanya kampeni nchi nzima; huwezi kushiriki uchaguzi na kufanya vizuri," alisisitiza Lissu.

Kiongozi huyo wa Chadema anakiri waziwazi kuhusu matatizo makubwa yanayokabili Chadema katika maandalizi ya kampeni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hapa anaonesha jinsi chama hiki kinavyokumbana na wakati mgumu katika medani za siasa katika siku za hivi karibuni.

## HIZI FEDHA ZINATOKA WAPI?

Lissu anashangaa wakati chama chao hakina fedha za kusimamisha wagombea sehemu kubwa ya nchi, lakini kuna fedha lukuki anazoziita chafu ingawa anadai hajui zinapotoka, zinazomwagwa kwenye kampeni za chaguzi zao za ndani!

"Wanachama wetu wakikamatwa, hatuna fedha za kuwasaidia, tukitaka kufanya mikutano fedha za maandalizi hakuna, lakini kwenye chaguzi zetu za ndani kuna mahela mengi yanamwagwa, nataka tuulizane Je, ni za kwetu?" Alihoji Lissu akiongea kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa Chadema Mkoa wa Singida, Novemba 13, 2024.

## CHADEMA HAIJAWAJENGEA UWEZO WANACHAMA

Wakati Lissu akinena hayo aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk. Willibrod Peter Slaa, amekosoa vikali viongozi wa sasa wa chama hicho kwa kushindwa kuwaongoza wananchi ipasavyo na kutokujenga uelewa wa kutosha juu ya wajibu wao wa kisiasa.

Akizungumza kupitia mtandao wa Clubhouse hivi karibuni, Dk. Slaa alieleza kuwa, Chadema imeshindwa kuwapatia wanachama wake ujasiri na uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa nchini, hali iliyosababisha wanachama hao kubaki katika hali ya kutojiamini na kutegemea zaidi uongozi wa chama kuliko kuwa na nguvu zao wenyewe.

>> INAENDELEA UK. 11

# Chadema, jahazi linalokwenda mrama

>> INATOKA UK. 10

Katika mazungumzo yake, Dk. Slaa alitilia mkazo umuhimu wa chama kuwa na mikakati ya kuwajengea uwezo wananchi, akieleza kuwa kwa muda mrefu wananchi wa Tanzania hawajawahi kupewa mwongozo madhubuti wa kujitegemea katika harakati za kisiasa.

"Usitegemee wananchi wawe mstari wa mbele, wanahitaji kuongozwa, Chadema mliwajengea uwezo? Upi? Kama mliwajengea uwezo wamefika wakashindwa kutekeleza, wananchi wajibu wao nini?" Alihoji Dkt. Slaa, akisisitiza kuwa ni jukumu la viongozi wa kisiasa kuwaongoza wananchi na kuwapa moyo wa kusimama kidete kwa ajili ya haki zao.

Dkt. Slaa alitoa mfano wa matukio mbalimbali ya siku za karibuni likiwamo tukio la Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha) kuchoma vitenge vilivyokuwa vimetolewa kama zawadi na Rais Samia Suluhu Hassan. Tukio kama hilo ni ishara ya namna chama kimeshindwa kuleta ushawishi wa kutosha kwa wananchi.

"Kwenye suala hili kwa mfano la kuchoma kanga na vitenge, wananchi hawakumwalika Rais Samia, nyinyi ndiyo viongozi mliomwalika, mngekwenda kama chama kwenda kumbana Samia kwamba ulitupa zawadi, sasa leo tunataka kuchoma hizi zawadi na mkachoma mbele yake? Wananchi mtawaingiza kwenye matatizo tu bila sababu," amesema Dkt. Slaa na kuongeza.

"Wananchi wana jukumu lao, wananchi mliwaomba kwenye maandamano wametokea. Wananchi wanahitaji kupewa ujasiri, na kauli za vyama vya upinzani juu ya maandamano zilitokaje?"

Aidha, Dkt. Slaa alizungumzia pia ukimya wa viongozi wa Chadema juu ya tuhuma zinazoelekezwa kwao za rushwa na ufisadi, akidai ukimya wao unamaanisha kuwa, kuna kitu kinaendelea ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani hapa nchini.

Ndipo wakaibuka John Mrema na Naibu Katibu Mkuu Bara wa chama hicho, Benson Kigaila wakikanusha vikali taarifa hizo za rushwa na ufisadi ndani ya chama chao!

Kama hiyo haikutosha, viongozi hao wakamshambulia vikali Makamu Mwenyekiti wao Tundu Lissu kwamba anatumika na CCM na serikali yake kuidhoofisha Chadema, lakini wakadai anajisumbua kwani hawatateteleka kwa propaganda hizo za kiongozi wao.

**WACHAPANA NGUMI ARUSHA**

Wakati malalamiko ya kuchezewa rafu katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji yakiendelea, wanachama wa Chadema walipigana ngumi hadharani jijini Arusha kwenye uchaguzi wa ndani wa chama hicho.

Baadhi ya wahanga wa ugomvi huo wa wenyewe kwa wenyewe walisema chanzo cha ngumi hizo ni Mwenyekiti wao wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema kutaka kupitisha kinyemela uongozi anaoutaka yeye Jijini humo!

Lema anadaiwa kukata baadhi ya majina ya wagombea waliokidhi sifa zote za kuwania uongozi na kuwapitisha wanaodaiwa ni mamluki wasio na sifa kwa masilahi yake binafsi.

"Kama hawa viongozi wetu wanailalamikia Serikali kwa kushirikiana na CCM kukata majina ya wagombea wa vyama vya upinzani kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mbona na wao wanafanya hivyohivyo kwenye chaguzi zetu?" Walihoji wanaChadema hao walioengulia kwenye uchaguzi huo wa Chadema uliofanyika Arusha wiki iliyopita.

Akijibu tuhuma hizo, Lema amesema vurugu zote zilizotokea Arusha zilipangwa na Benson Kigaila ili kumchafua yeye, kwani waliofanya tafrani hizo ni marafiki zake wakubwa.

Lema akizungumza na wanahabari mkoani Arusha Novemba 16, 2024 juu ya ugomvi huo wa wanachama wa chama hicho, alijibu kuwa, anayeweza akawa na majibu ya hilo ni Kigaila.

"Maneno haya isivyo bahati ninayasema, ila ninayasema kwa ajili ya sasa ukiniuliza mimi kwamba ile fujo chanzo chake ni nini? Naibu Katibu kashindwa kutunza uaminifu wangu, kwa sababu nyinyi wanahabari hamkurekodi lile jambo kwenye



vikao vya chama, haya nitayasema hadharani" Lema.

Mwenyekiti huyo wa Chadema Kanda ya Kaskazini, amesisitiza vurugu hizo zilizojitokeza wakati wa uchaguzi wa viongozi wa Mkoa wa Arusha, zilipangwa kwa lengo la kuharibu uchaguzi huo na kumchafua yeye.

Lema ameagiza viongozi wa mikoa na wilaya wanakotoka waliosababisha vurugu hizo, kuwasiliana na matawi wanayotoka na kuwavua uanachama kwa madai kuwa wamekidhalilisha chama hicho.

"Ninaagiza viongozi wa chama, kwa yeyote aliyehusika kwa sababu wapo waliotoka Mkoa wa Kilimanjaro, walikuja kufanya fujo na kusababisha taharuki kubwa na udhalilishaji kwa chama chetu, wachukuliwe hatua za kuvuliwa uanachama katika matawi yao mara moja kwa sababu wamekidhalilisha chama," amekaririwa Lema.

Lema amesema alipanga kutozungumza juu ya suala hilo ila amelazimika kufanya hivyo, baada ya kuona anachafuliwa jina lake pamoja na suala hilo kuleta taharuki kwa wanachama.

VIKAO VYA SIRI

Hata hivyo, miongoni mwa anaowalaumu Lema mkoani Arusha wameubuka na kudai Lema anakutana hufanya vikao vya siri na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda na mbunge wa Jimbo hilo, Mrisho Gambo.

Ukisikia jahazi kwenda mrama ndiyo hali hii sasa wanayopitia Chadema, wakifanya mchezo tu, watakizamisha 'chombo' baharini!

Na malalamiko yote watayahamishia CCM, wakati wao wenyewe ndiyo wanaotoboa mtumbwi wao mchana kweupe tena hadharani kama panya!

Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.



# Rais Dk. Samia ametuheshimisha kualikwa G 20



**Na Hamid Yassin**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan alikuwa kwenye ziara ya kikazi nchini Brazil kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Kundi la G20 uliofanyika kuanzia juzi Novemba 18 hadi jana, Novemba 19 jijini Rio de Janeiro, Brazili.

Taarifa iliyotolewa na Serikali wiki iliyopita ilisema kuwa, Rais Dk. Samia alialikwa na Rais wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva ambaye pia ni Mwenyekiti wa G20 kushiriki mkutano wa Jukwaa hilo lenye lengo la kukuza ushirikiano wa kimataifa kwenye masuala ya kiuchumi.

Hii ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuhudhuria katika mkutano wa G20. Mwaliko huu unatokana na heshima na ushawishi mkubwa ambao Rais Dk. Samia amejijengea kwenye majukwaa ya kimataifa.

Pamoja na mambo mengine, katika mkutano huo, Dk. Samia alishiriki mijadala inayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika mapambano dhidi ya njaa, umasikini, kuchochea maendeleo endelevu na matumizi ya nishati mbadala.

Rais Samia alitumia jukwaa hilo linalokutanisha nchi zenye uchumi mkubwa zaidi duniani kuelezea jitihada zinazofanywa na serikali yake kuhakikisha usalama wa chakula, kupunguza umaskini, kujenga maendeleo endelevu na kutafuta fursa za ushirikiano zinazowaletea ustawi Watanzania kupitia sekta za uzalishaji.

Pia akiwa Brazil, Dk. Samia alifanya mikutano ya pembezoni na taasisi kubwa za kifedha duniani pamoja na kukutana kwa mazungumzo na Wakuu wa nchi na serikali pamoja na baadhi ya nchi wanachama wa G20 akiwemo mwenyeji wake, Rais wa Brazili.

Lengo la mazungumzo hayo ni kukuza na kuimarisha uhusiano wa nchi hizi mbili, hususani kwenye sekta za viwanda, biashara, kilimo, nishati, utalii na pamoja na kutafuta fursa mbalimbali za ushirikiano, uwekezaji na miradi ya pamoja.

Ushiriki wa Rais Dk. Samia kwenye mkutano huu wa G20 unalenga kuhakikisha pia Tanzania inaendelea kuchangia ipasavyo mijadala muhimu ya kimataifa kuhusu maendeleo duniani na kunadi sera za uchumi za kimataifa zitakazochochea maendeleo na ustawi zaidi Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

**R4 ZA DK. SAMIA**

Dk. Samia alipoingia madarakani Machi 19, 2021, alikuja na falsafa ya R4, moja ya hizo R4 ni ile ya 'Reform' ambayo inamaanisha mageuzi.




Miongoni mwa mageuzi aliyoyafanya Rais wetu ni yale ya sera ya kidiplomasia.

Yaani kutumia ushirikiano wa nchi kuweza kudumisha na kujenga diplomasia ya kimataifa. Hivyo cha kwanza kilichochangia kupata mwaliko huu ni uwezo wake wa ushawishi kwenye majukwaa ya kimataifa.

Tanzania katika jukwaa la kimataifa tangu tujipatie uhuru enzi ya Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Nyerere unaweza kusema bila kusita kuwa ndiye 'Kaka mkubwa' kwenye eneo hili la diplomasia ya kimataifa barani Afrika, hivyo anachofanya Dk. Samia ni kuhuisha sehemu zilizolegalega.

Tanzania Kusini mwa Jangwa la Sahara Mwalimu alisaidia uhuru wa mataifa mengi ndiyo maana nasema hapa sisi ndiyo 'Kaka mkubwa' wa diplomasia kwenye bara hili, hivyo haishangazi hata kidogo Dk. Samia kualikwa kule Brazili kwa vile amerudisha uhusiano wa kimataifa katika miaka yake hii mitatu na nusu madarakani.

Ukisoma mkakati wa sera yetu Tanzania ya mambo ya nje ya mwaka 2021 na ile ya mabadiliko ya mwaka 2023, inazungumza namna gani nchi itaweza kutumia mikakati ya kushiriki kwenye mikutano na majukwaa ya kimataifa, kama vile jumuiya ya kimataifa na Umoja wa Afrika.

Huo ni mwendelezo wa Tanzania katika kuwa sehemu ya kupanga, kutatua na ya kupitisha changamoto mbalimbali za kimataifa.

Hii ni pamoja na masuala mbalimbali yanayotokea duniani kama mabadiliko ya tabianchi, mdororo wa kiuchumi, changamoto za vita na maendeleo ya sayansi na teknolojia kama matumizi ya 'akili mnemba'.

**DK. SAMIA ALIDHAMIRIA**

Akiwa na miezi kadhaa tangu kuingia madarakani, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alihutubia Mjadala Mkuu wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kwenye Makao Makuu yake jijini New York, Marekani, ikiwa ni mara ya kwanza tangu ashike wadhifa huo mwezi Machi mwaka 2021.

Hapo akawa anamulika masuala mbalimbali kuanzia uchumi, siasa, tabianchi, usawa wa jinsia na janga la Covid – 19 lililokuwa linapamba moto wakati huo.

Rais Samia katika hotuba yake ya kwanza ana kwa ana kwenye mjadala huo, kiuchumi na kidiplomasia ilifafanuliwa kuwa na maana kubwa na muhimu kwake.

Hapo akaanza na dhana ya ushirikiano wa kimataifa, akitamka katika ujumbe uliotoa mvuto kwa kusema; "Chini ya uongozi wangu, Tanzania itaendelea kuwa mshirika muhimu wa Umoja wa Mataifa na muungaji mkono wa kutegemewa wa suala la ushirikiano wa kimataifa.

"Tutanyoosha mkono kwa wale wanaotukumbatia na kushirikiana nasi. Tutaendelea kuwa Tanzania ambayo mmeifahamu kwa muda mrefu.

>> INAENDELEA UK. 13

# Dk. Samia ametuheshimisha kualikwa G 20

>> INATOKA UK. 12

"Tanzania yenye amani na ambayo inashirikiana na nchi zote kubwa au ndogo, zenye nguvu au zisizo na nguvu, tajiri au masikini kuifanya dunia yetu kuwa bora kwa ajili yetu sote."

Ushuhuda na mwendelezo wa ahadi ya kwanza na mwendelezo wa utekelezaji wa mialiko, sasa anapata mialiko mingi kimataifa, inayombebesha heshima kimataifa duniani, na ndiyo tunaona alikuwa jijini Rio De Janeiro Brazil, kwa siku mbili.

Huo ni mkutano wa viongozi wa kundi la nchi 20 zenye uchumikubwa duniani, mwaliko ukitolewa na Mwenyekiti wao, Rais Luiz Inacio Lula da Silva wa Brazil, huku Dk. Samia akiweka rekodi kuwa Rais wa kwanza mwanamke kuhudhuria mkutano wa viongozi wa kundi hilo, tangu kuitwa G20 mwaka 2009, ikipanda kutoka kundi la nchi nane, G8.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaonesha kuwa marais wastaafu nchini Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete, walishiriki mikutano ya G8 iliyofanyika mwaka 2005 na 2008.

Kundi la G20 linaundwa na mataifa ya Argentina, Australia, Brazil, Canada, China, Ufaransa, Ujerumani, India, Indonesia, Italia, Japani, Jamhuri ya Korea, Mexico, Russia, Saudi Arabia, Afrika Kusini, Uturuki, Uingereza na Marekani.

Pia, kuna wanachama wa kitaasisi; Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Ulaya (EU), ambao mara nyingi unawakilishwa na rais wake.

Vilevile kuna wadau; taasisi zinazowakilishwa na watendaji wake wakuu, ambazo ni Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia (WB), pia Kamati ya Maendeleo ya IMF na Benki ya Dunia.

Aidha, kimuundo G 20 hufanya kazi bila ya sekretarieti ya kudumu wala wafanyakazi na uenyekiti wake huzunguka kila mwaka, kati ya wanachama na mwenyekiti anatokana na mmoja wa mataifa waasisi.

Mwenyekiti aliyeko, huunda sekretarieti ya muda kwa wakati wake, inayoratibu kazi ya kikundi na inapanga mikutano yake.

Pia, Umoja wa Afrika (AU) umejumuishwa kuwa mwanachama wa kudumu katika muungano G20 katika mkutano uliokamilika nchini India mwaka jana na sasa una hadhi sawa na Umoja wa Ulaya (EU).

Viongozi wa mataifa wanachama wa G-20 hukutana kila mwaka mara mbili katika Kongamano la G-20.

**MIKUTANO G20**

Kihistoria makongamano ya G-20, yalianzishwa ikiwa ni mwitikio wa tatizo la fedha kati ya mwaka 2007 hadi 2010 na pia kuonekana kama nchi zinazostawi hazikujumuishwa vya kutosha katika majadiliano ya kiuchumi duniani.

Makongamano ya G-20 ya wakuu wa nchi au serikali yalifanyika mbali na mikutano ya G-20 iliyohusisha mawaziri wa fedha na magavana wa benki kuu. Hawa waliendelea kukutana kuandaa kongamano la wakuu wa nchi, pia kutekeleza maamuzi yao.

**SAFARI ZA DK. SAMIA**

Tangu aingie madarakani miaka mitatu na nusu sasa Rais Samia amefanya ziara kadhaa ambazo zimekuwa na faida kubwa kwa nchi yetu.

Apirili mwaka 2021 Rais Samia alifanya ziara za kujenga uhusiano katika nchi jirani na hata kushuhudia chaguzi katika nchi za Afrika Mashariki, Uganda, Kenya, Burundi na huko Msumbiji katika kikao cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).



Katika ziara hizo, baadhi ya maeneo kama Burundi amefika zaidi ya mara moja na baada ya nusu mwaka kuanzia mwezi Julai, pia amefika nchi za Malawi, Rwanda na Zambia alikohudhuria matukio muhimu.

Baadaye kuanzia mwezi Septemba ya mwaka huo 2021, Rais Dk Samia alifika katika mataifa ya Marekani, Uingereza, Misri na Uskochi (Scotland).

**MWAKA 2022**

Ni mwaka ambao alizuru nchi zaidi ya 15 akiwajibikia nchi yetu kiuchumi na na kujenga diplomasia ya uhusiano mwema, huku akiwa na mvuto uliompatia mialiko mingi kimataifa.

Hapo kunatajwa mataifa kama Msumbiji, Ufaransa, Ubelgiji kwenye kikao cha pamoja cha AU na EU, pia akafika Jamhuri ya Emerati (UAE) kwenda kuimarisha biashara ya nchi, Marekani akaenda kuzindua Sinema ya Royal Tour katika majiji ya Washington, New York na Los Angeles, mchakato uliochukua zaidi ya wiki, sasa 'ikijibu' katika biashara ya utalii kimataifa.

Baadaye akawa katika ziara za uhusiano kati ya mwezi Mei na Julai huko Kampala, Uganda; Accra Ghana, Muscat, Oman; na Dakar Senegal.



Kuanzia mwezi Agosti akajumuika na wakuu wa nchi za SADC huko Kinshasa, DRC, pia akawapo katika uchaguzi mkuu wa nchini Kenya mwezi uliofuata na maziko ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza, ikizingatiwa Tanzania ni tabaka la Jumuiya ya Madola.

Safari ya Rais Dk. Samia mwezi huo ikamfikisha Msumbiji, safari hiyo akiwa makao makuu Maputo na ziara ya 2021, alikuwa Pemba kunakoathiriwa na hali ya hewa.

Oktoba akawa Doha, Quatar kwa kikao mahsusi kuhusu afya ya umma na dunia, kisha mwezi Novemba akaendeleza uhusiano na ndugu wa taifa walioko Beijing, China na kurejea kikao cha hali ya hewa (COP) kama kinachoendelea hivi sasa kwa mwaka huu, hadi tarehe 22. Kufika mwezi Desemba, Rais Dk. Samia alikuwa Marekani katika mkutano wa viongozi duniani.

**MWAKA 2023**

Mapema mwaka jana. Rais alikuwa Davos Uswisi, kujadili uchumi wa dunia, kisha akarejea kikaoni kwa Waafrika wenzake huko, Dakar Senegal alikokanyaga kwa mara ya pili. Baadaye, Februari Rais akawapo katika kikao cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Bujumbura, Burundi na huko akawapo Addis Ababa, Ethiopia kwa kikao cha AU.

Pia, akawa na ziara za Afrika Kusini, Windhoek, Namibia, Uganda, Nigeria kwenye uchaguzi, akakanyaga tena nchini Malawi kwenye uchaguzi, Mnamo Agosti akawa Johannesburg, Afrika Kusini, ilipofika Septemba akahudhuria kikao cha hali ya hewa.

Pia, kukawapo kikao cha kilimo cha kisasa huko Doha, Quatar na akaendeleza uhusiano ziarani India mwezi huo wa Oktoba, hali kadhalika Zambia. Dk. Samia kaendeleza ziara hizo, akihudhuria kikao cha utalii duniani nchini Rwanda na akarejea kikao cha wakuu wa nchi wa SADC huko Luanda, Angola, kikao cha uwekezaji wa Benki ya Afrika huko Morocco na Mkutano wa Afrika, Saudi Arabia.

Kisha akarejea Uarabuni UAE kuhudhuria kikao cha hali ya hewa, kilichoanza mwishoni mwa Novemba na kumalizika Desemba.

**MWAKA 2024**

Taarifa za safari za rais mwaka huu zinagusa nchi za Indonesia kudumisha uhusiano, makao makuu ya katoliki Vatican City, pia Norway; kwenye kikao cha AU huko Addis Ababa, Ethiopia, Windhoek, Namibia, Uturuki, Kenya (mkutanoni) na Ufaransa.

Pia, kuna ziara tofauti za Afrika Kusini na Rwanda, kwenye matukio ya uchaguzi; vikao vya SADC huko Zimbabwe na AU nchini Kenya katika mwezi huo wa Agosti.

Mwezi Septemba amehudhuria kikao cha uhusiano wa Afrika na China, kilichofanyika huko Beijng China na hivi karibuni alikuwa na kikao kingine Marekani.

**Kwa ushauri na maoni; 0768 888 787 ama 0784 122 020.**

# Ripoti: Wanaume wanakufa kwa wingi na Ukimwi kuliko wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

WANAUME wengi nchini Kenya wanakufa sana kwa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Ukimwi na magonjwa yanayoandamana na virusi hivyo ikilinganishwa na wanawake, licha ya kwamba kwa upande wa wanawake maambukizi ni makubwa kuliko wanaume!

Takwimu kutoka Baraza la Kitaifa la Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza la Kenya (NSDCC) zinaonyesha kuwa zaidi ya watu milioni 1.38 wanaishi na vizuri vinavyosababisha Ukimwi nchini humo huku wanaume wakiwa ni asilimia 35 sawa na watu 487,710 na idadi iliyobaki, yaani asilimia 65 wakiwa wanawake.

Taarifa iliyochapishwa na gazeti la Taifa Leo, inaonesha kwamba licha ya kuwa idadi ya wanaume wanaoambukizwa Ukimwi (asilimia 2.2) ni ndogo ikilinganishwa na wanawake (asilimia 4.5), wanaume ndio wengi huaga dunia kutokana na virusi hivyo hatari kulinganisha na wanawake, utafiti umeonesha.

Mnamo mwaka 2023, wastani wa wanaume 26 walikufa kila siku nchini Kenya kati ya idadi ya vifo 56 ambavyo vilisababishwa na ukimwi na magonjwa mengine yanayoandamana na virusi hivyo.

### KUTOKWENDA HOSPITALI

Naibu Mkurugenzi wa NSDCC, Caroline Kinoti anasema sababu kubwa ya wanaume kufa sana kutokana na virusi hivyo ni kutokana na kutokwenda hospitalini, hali inayosababisha virusi kuwa na nguvu zaidi kisha kupanda hadi viwango vya juu.

"Kinyume na wanawake ambao huenda hospitalini mara nyingi kikla wanapokuwa wajawazito. Kutokana na sera ya kila mjamzito kupimwa ukimwi imekuwa sababu muhimu ya wapo kupimwa na kujua hali zao.

"Lakini kwa upande wa wanaume huenda tu hospitalini wakilemewa na maradhi. Hapa ndipo wao hubainika wana maambukizi ya virusi vya ukimwi na mara nyingi huwa wameshachelewa sana," anasema Kinoti na kuongeza hata hivyo kwamba katika mazingira ya kawaida, wanawake wamekuwa wakijitokeza kupima virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukumi kulinganisha na wanaume.

Anasema ingawa idadi ya wanaume ambao wanatumia vidonge vya ARVs imepanda kutoka asilimia 81 mnamo 2020 hadi asilimia 90 mnamo 2023, wanaume pia hukumbana na changamoto za matumizi ya dawa za kulevya, uhalifu na pia huwa hawashiriki mipango ya afya ya kuzuia maradhi mbalimbali kulinganisha na wanawake.

Mnamo mwaka 2023, Kenya ilikuwa na maambukizi mapya 16, 752 ya ukimwi huku wanaume wakiwa 4,072. Watu ambao wapo katika umri wa kati ya miaka 15-34 walijumuisha asilimia 73 za maambukizi yote.

Kwa mujibu wa gazeti la Taifa leo, nchini Kenya kaunti zenye maambukizi mengi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa ukimwu ni Kisumu, Homa Bay, Migori, Siaya, Nairobi, Nakuru, Kiambu, Busia na Mombasa ambazo zilichangia asilimia 51 za maambukizi mapya ya ukimwi mwaka jana.

### HALI ILIVYO TANZANIA

Hakujafanyika utafiti wa kina kuangalia ni akina nani wanakufa zaidi kwa upande wa wanawake na wanaume wanaoishi na VVU, lakini kama ilivyo kwa Kenya, hata Tanzania, wanawake wanabeba mzigo mkubwa wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ikilinganishwa na wanaume.

Takwimu zinaonesha kuwa kiwango cha maambukizi ya VVU ni asilimia 6.3 kwa wanawake, wakati kwa wanaume ni asilimia 3.4. Hali hii inatokana na sababu mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kibaolojia:

Kwa sababu za kibaolojia, wanawake wana uwezekano mkubwa wa kupata maambukizi ya VVU wakati wa kujamiiana kwa sababu ya muundo wa maumbile yao, ambao hufanya uwezekano wa maambukizi kuwa mkubwa zaidi ikilinganishwa na wanaume.

Kwa upande wa kijamii na kiuchumi umaskini unawalazimisha baadhi ya wanawake kuingia katika tabia hatarishi kama vile ukahaba au kutegemea msaada wa kifedha kutoka kwa wanaume, ambao mara nyingine huwajumuisha katika mahusiano yasiyo salama.

Wanawake wanakosa uwezo wa kujadiliana matumizi ya kinga (kondomu) katika mahusiano, hasa katika jamii zinazodhibitiwa na mfumo dume.

Tanzania inatajwa kuwa miongoni mwa nchi ambazo bado zina viwango vya juu vya ndoa za utotoni, ambavyo huongeza hatari ya maambukizi kwa wasichana wadogo walio na wenzi wa umri mkubwa wenye maambukizi.

Unyanyasaji wa Kijinsia ikiwa nji pamojka na ubakaji na ukatili wa kingono, ni changamoto nyingine inayowaweka wanawake katika hatari kubwa ya kuambukizwa.

### HALI YA MAAMBUKIZI TANZANIA

Kiwango cha maambukizi ya VVU nchini Tanzania kimekuwa kikishuka taratibu. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, kiwango cha maambukizi kwa watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi kimepungua, likiwa asilimia 4.7 kitaifa.

Sababu za hali hii ni pamoja na maendeleo ya afya. Kwamba ongezeko la watu wanaotumia dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) limechangia kupunguza maambukizi mapya. Watu waliofubaza virusi kwa sasa ni takriban asilimia 78 ya walio na maambukizi, hivyo kupunguza hatari ya kueneza virusi.

Kuhusu maeneo yenye maambukizi zaidi ya VVU ni pamoja mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inayohusisha Njombe, Iringa, na Mbeya. Njombe inaongoza kwa maambukizi ikiwa na iwango cha asilimia 12.7, ambacho ni mara mbili ya kiwango cha kitaifa.

Sababu za maambukizi makubwa katika mikoa hii zinatajwa kuwa ni pamoja na mtawanyiko wa wakazi, tamaduni, na changamoto za kimaisha zinazochangia tabia hatarishi.

### TIBA YA UKIMWI

Hadi sasa, bado hakuna tiba kamili ya ugonjwa wa Ukimwi, lakini maendeleo makubwa yamefikiwa katika utafiti na mbinu za kudhibiti virusi vya VVU.

Mosi ni tiba za upandikizaji wa uloto au uboho: Wagonjwa wachache waliopata upandikizaji wa uloto wameripotiwa kupona kabisa VVU. Ingawa hii ni hatua ya matumaini, mbinu hii bado ni hatari, ghali, na haifai kutumika kwa kiwango kikubwa.

Pili, chanjo ya majaribio: Utafiti wa chanjo umeendelea kuimarika, na baadhi ya nchi kama Tanzania zinafanya majaribio ya chanjo zinazolenga kuzuia maambukizi mapya ya VVU. Chanjo hizi ziko katika hatua za pili za majaribio na zinatarajiwa kuleta matokeo mazuri.

Tatu, Matumizi ya dawa za kupunguza makali (ARVs): Dawa hizi zimekuwa msaada mkubwa kwa watu wanaoishi na VVU, zikisaidia kufubaza virusi hivyo na kupunguza hatari ya maambukizi mapya. Kiwango cha watu waliopunguza makali ya virusi kimeongezeka, na wengi wanaweza kuishi maisha yenye afya.

Nne, maendeleo ya kisayansi na tafiti mpya: Mikutano ya kimataifa inaendelea kuonesha matumaini ya kufanikisha tiba, huku wanasayansi wakichunguza teknolojia mpya na mbinu za kutibu VVU.

Kingine cha muhimu ni kwamba kinga bado ni njia bora zaidi ya kudhibiti maambukizi ya VVU. Kuna tatizo kwamba sasa hivi ugonjwa huu hauzungumzwi sana na watu wanadhani umekwisha wakati bado upo na unaendelea kutesa watu wengi.

Kingine cha kugusia, ni pale unapogundulika kuugua ugonjwa huu ni muhimu kufuata masharti ya madaktari watalaamu wa lishe na kutumia dawa za kufubaza VVU kwani ndizo zinasaidia watu wengi kwa sasa. Epuka kutegemea maombi na waganga wa jadi na tiba mbadala matapeli.



# Serikali ichukue maamuzi magumu itakachogundua kadhia ya Kariakoo

**Na Mwandishi Wetu**

KWANZA nianze kwa kuwapa pole wale ambao wamepoteza ndugu na wapendwa wao katika ajali ya kuporomoka kwa ghorofa katika mtaa wa Kongo na Mchikichi, Kariakoo, wilayani Ilala, Dar es Salaam.

Pia ninawapa pole waliojeruhiwa katika ajali hiyo na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu wapone haraka na maisha yaendelee.

Ninawapongeza wote walioshiriki katika zoezi la uokoaji ambalo linaelezwa kwamba ni gumu sana lakini watu wameendelea kupambana hata baada ya Rais Samia kuongeza muda wa kuokoa watu kwa mikono baada ya saa 72 zinazotajwa kumalizika. Hongereni sana wapambanaji.

Ni kweli, kuna ajali zinazotokana na majanga ya asili ambazo si rahisi kuzizuia. Kwa mfano kuna klipu moja nimewahi kuiona, na kama sikosei ni katika jiji la Paris, Ufaransa, ambako mafuriko yanaoneka yakisomba hadi maghorofa.

Lakini hili lililotukuta Tanzania lina kila dalili ya uzembe wa mwanadamu, kutokana na yale ambayo watu wamejionea na hata kuyazungumzia.

Ninafahamu kamati maalumu imeundwa kuchunguza kwa kina nini hasa kimesababisha ghorofa hilo kuporomoka na hata kitengo cha maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kinachunguza kujua sababu ya kilichotokea.

Hatua ya kuunda kamati hiyo imetokana na maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye pia ametaka kukagua hali ya kimuundo ya majengo yote jijini Dar es Salaam na hasa katika eneo la Kariakoo lenye shughuli nyingi.

Ni jambo la kumpongeza sana Rais Samia ambaye licha ya kuwa nje ya nchi akishiriki katika Mkutano wa Viongozi wa G20 mjini Rio de Janeiro, ameuhakikishia umma kuhusu shughuli ya uokoaji kufanyika kwa kiwango kinachotakiwa.

"Baada ya tukio hili la kusikitisha, namuagiza Waziri Mkuu aongoze timu ya wakaguzi wa majengo kuendelea na ukaguzi wa kina wa majengo yote ya eneo la Kariakoo, ili tuweze kupata tathmini ya kina ya hali yake ya kimuundo," alisema Rais Hassan.

Aidha Rais alitangaza kwamba polisi watakusanya taarifa kamili kutoka kwa mmiliki wa jengo lililoporomoka kuhusu ujenzi wake.

Imeelezwa pia kwamba matokeo ya uchunguzi yatatolewa hadharani, huku serikali ikisema itachukua hatua zozote muhimu kulingana na matokeo.

Serikali pia imeahidi kulipia gharama za matibabu kwa majeruhi na kuhakikisha kuwa walioaga wanashughulikiwa kwa heshima inayostahili.

Pamoja na kusuburi matokeo ya uchunguzi wa kina, yapo madai kwamba majengo mengi Kariakoo, kutokana na tamaa, wamiliki wake wamekuwa wakiyaongezea vyumba kwa kuchimba chini kinyemela au wakati mwingine kuongeza juu sehemu ili kupata vymba zaidi vya kupangisha wafanyabiashara.

Inasemekana maeneo kama mtaa wa Kongo, vyumba vya biashara au kuhifadhia mizigo kodi yake inaanzia shilingi milioni tatu hadi tano kwa mwezi na hiki ndicho huwafanya wafanyabishara kutaka na kutaka zaidi.

Baadhi ya majengo haya inadaiwa kwamba ni ya siku nyingi, na hayakujengwa kwa ajili ya kuhimili mzigo mzito lakini kwa ajili ya tamaa watu wanafanya ndivyo sivyo. Jengo lililopromoka, limedaiwa pia kwamba lilizidiwa na mizigo.

Hapa kuna maswali mengi kuhusu wahusika kwa maana ya mamlaka za serikali za mitaa kama Halmashauri ya Wilaya ya Ilala kama wanaridhia kuitoa vibali vya kuruhusu upanuzi wa majengo kwa njia zisizofuata kanuni za ujenzi stahiki. Tena watu wanajenga huku watu wakiendelea na biashara zao.

Ni vyema Tume itakapoleta taarifa serikali isimwangalie nyani usoni bali kuchukua maamuzi magumu ya kuvunja maghorofa yote yatakayoonekana ni hatarishi. Wafanyabishara watakapotakiwa kupisha ubomoaji wa maghorofa hatarishi wewe tayari kupisha.

Pia kama kuna watu walitoa vibali ama wanazembea watu kufanya ujenzi bila kufuata taratribu basi ni vyema wachukuliwe hatua kali sana ili kuhakikisha mambo kama haya hayatokei tena katika nchi yetu.

Hofu yangu na baadhi ya Watanzania wenzangu ni baada ya ripoti kutoka wahusika kuona ugumu wa kuchukua maamuzi magumu!

Zipo taarifa zinazoneesha kwamba suala la tume kuundwa na kugundua kwamba katika jiji la Dar es Salaam kuna takribani majengo 100 ya ghorofa yaliyojengwa kinyume cha taratibu za ujenzi si la leo na hata Bunge liliwahi kuelezwa huko nyuma.

Hii ni kwa mujibu wa ripoti iliyoundwa na aliyekuwa Waziri Mkuu na kisha kujiuzulu, Hayati Edward Lowassa ambapo ilidaiwa kwamba kati ya maghorofa 505 ambayo yalikaguliwa, majengo 147 yalikutwa wakati huo yakiwa hayana nyaraka za ujenzi.

Lowassa aliunda tume baada ya jengo la hoteli ya Chang'ombe Village Inn, lililokuwa maeneo ya Keko, kuanguka ghafla mwaka 2006. Katika tukio hilo, mtu mmoja alikufa na wengine kadhaa walijeruhiwa.

Wakati wa tukio hilo, kuliibuka madai kwamba kulikuwa na ukiukwaji katika ujenzi wa ghorofa hilo, jambo ambalo lilimsukuma Lowassa, kuunda tume haraka ya kukagua ghorofa zote zilizopo jijini Dar es Salaam.

Aliyekuja kuchukua nafasi ya Lowassa – Mizengo Kanyanza Pinda, baadaye aliliambia Bunge kuwa "Tume ya ukaguzi ya Lowassa," ilibaini pia ghorofa 81 zilikiuka masharti ya ujenzi na akasema, kwa mujibu taarifa zilizopo kwamba ghorofa zingine 22 wamiliki wake hawakupatikana na zilijengwa bila kuzingatia taratibu na sheria za ujenzi.


Hakuna anayeweza kusema hatua zilizochukuliwa toka muda huo. Lakini katika hili la sasa ninaamini kwamba safari hii viongozi wetu hawataacha kuchukua maaamuzi magumu ya kuwawajibisha wote ambao wamekuwa chanzo cha ghorofa kujengwa au kuwepo bila kuwa ithibati sahihi na kubomoa maghorofa yote yatakayoonekana kwamba ni hatarishi kwa maisha ya wanadamu.

Lakini pengine ni wakati mwafaka pia wa kufikiria kuanzisha 'Kariakoo' nyingine moja au zaidi kwa maana ya kuanzisha miji mingine mithili ya Kariakoo (Satellite Cities) katika jiji la Dar es Salaam.

Satellite cities ni miji midogo iliyojengwa karibu na jiji kuu (mara nyingi umbali wa kilomita chache hadi kadhaa) na iliyoundwa kusaidia kupunguza msongamano wa watu, shughuli za kiuchumi, na makazi ndani ya jiji hilo kuu.

Mara nyingi, miji hii ina miundombinu yake ya kiuchumi, kijamii, na utawala lakini inahusiana kwa karibu na jiji kuu, ambalo hufanya kama kitovu cha shughuli za kanda hiyo.

Kuna wakati Kigamboni ilikuwa inafikiriwa kuendelezwa kama Satellite City na wakati mwingine eneo la Kibamba lilitajwa. Sijui mkakati huo uliishia wapi. Hili litukumbushe kuanzisha kitu kama hicho ili kupunguza msongamano Kariakoo na kupunguza tamaa. Tutake tusitake, Kariakoo imejaa na tunahitaji Kariakoo mpya na haraka!



# Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

### KUELEKEA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA:

# Tuwasikilize wagombea, tuchague kwa usahihi

SIKU zimekwisha. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa umekaribia. Ndugu mwananchi na msomaji wangu, hivi unajua kuwa Jumatano ijayo Novemba 27, 2024 ndiyo siku ambayo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hapa nchini unatarajiwa kufanyika? Kama ulikuwa hujui au umesahau basi habari ndiyo hiyo. Jiandae. Katika uchaguzi huu, wananchi waliojiandikisha kwenye daftari la wakazi la wapiga kura watatimiza haki yao ya kikatiba ya kuwachagua viongozi katika vijiji, vitongoji na mitaa yao. Uchaguzi huu unaongozwa na kaulimbiu isemayo "Serikali za mitaa, sauti ya wananchi, jitokeze kushiriki uchaguzi."Ni vyema ifahamike kuwa mojawapo ya madhumuni ya kuwepo kwa serikali za mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi.

Kimsingi, serikali ya mtaa ndiyo ngazi ya kwanza ya utawala inayomfikia mwananchi kwa ukaribu zaidi pale alipo kwani inatoa huduma kwa ukaribu zaidi kabla ya kuhudumiwa na serikali kuu. Kwa lugha nyingine ndicho kiungo baina ya wananchi na serikali yao kuu.Mipango ya maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi inaanzia katika mtaa, kitongoji au kijiji anachoishi mwananchi.

Ni muhimu kwa wananchi kuitumia fursa hii adhimu inayojitokeza kila baada ya miaka mitano kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu kuchagua viongozi wa serikali za mitaa ili wawe kiungo muhimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa ustawi wa maisha ya wananchi.Zoezi la uandikishaji wapigakura lilikwishakamilika. Wananchi waliojitokeza kujiandikisha ndiyo wenye sifa za kupiga kura. Sasa kama hukujiandikisha, nikupe pole. Ni wale waliojiandikisha tu ndiyo wenye sifa ya kupiga kura Novemba 27, 2024.

Kwa mwananchi aliyejiandikisha, kazi bado haijaisha. Kwa nini? Kwa sababu kujiandikisha ni jambo moja na kupiga kura ni jambo jingine, Aliyejiandikisha analo jukumu la kusikiliza sera za wagombea kutoka vyama mbalimbali vya siasa ili aweze kufanya maamuzi sahihi ili siku atakapokwenda kwenye kituo cha kupiga kura aweze kufanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi bora, wazalendo, wachapakazi na wenye kujituma kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, enzi za uhai wake aliwahi kusema "Msiwachague viongozi kwa vile wanajua kunena maneno mazuri au kwa sababu wanapendwa na wengi, angalieni moyo wao, nia yao na matendo yao." Jambo hili linapaswa kuzingatiwa sana na wapiga kura.




Ni muhimu kwa wananchi waliojiandikisha kupiga kura kutenga muda kwenda kwenye mikutano ya hadhara kusikiliza sera za wagombea. Wasikilize mipango na mikakati waliyonayo wagombea katika kujenga ustawi wa wananchi. Kama mwananchi ataridhika na sera, nia na maono ya mgombea fulani, ndipo afanye maamuzi sahihi ya kumchagua mgombea huyo.

Maamuzi ya kumchagua mgombea fulani hayapaswi kuwa maamuzi ya kukurupuka au ya mazoezi bali yanapaswa yawe maamuzi yanayotokana na tafakuri ya kina iliyoambatana na kuchakata sera na maono ya wagombea kadhaa aliowasilikiza katika majukwaa wakijinadi sera zao, ndipo atakapokuwa katika nafasi nzuri ya kufanya maamuzi sahihi.

Viongozi watakaochaguliwa katika uchaguzi huu ndiyo watakaoingia katika jukumu la kuwahudumia wananchi kuanzia mwaka huu 2024 hadi 2029. Kipindi hiki cha miaka mitano kinaweza kuwa kitamu au kichungu kwa wananchi kutegemea na aina ya viongozi watakaochaguliwa.

Naamini hakuna mwananchi anayetaka miaka mitano iwe michungu, lakini ikumbukwe kuwa njia ya kufanikisha miaka mitano ya neema iliyoambatana na maziwa na asali katika mtaa, kijiji au kitongoji chake ni kuchagua viongozi bora, wazalendo na wachapakazi.

Viongozi wa dini na wa kimila wanayo nafasi kubwa ya kushirikiana na serikali na wadau wengine katika kuhamasisha waumini na wananchi wao kupiga kura ili kuchagua viongozi wa serikali za mitaa. Hata fedha za miradi ya maendeleo kama vile elimu, afya, maji, masoko zinazotolewa na serikali kuu zinawafikia viongozi wa serikali za mitaa katika usimamizi na ufuatiliaji ili thamani ya fedha iweze kuonekana na hatimaye wananchi wanufaike na miradi hiyo inayotekelezwa katika maeneo yao.

Nihitimishe kwa kukushauri ewe mwananchi mwenzangu uliyejiandikisha, kuweka ratiba zako vizuri ili siku ya uchaguzi uweze kutimiza haki yako ya kikatiba ya kupiga kura bila uwepo wa kisingizio chochote.

Kwa kutambua umuhimu na unyeti wa uchaguzi huu, serikali imeamua kuifanya siku ya uchaguzi huu kuwa ya mapumziko ili kutoa fursa kwa wananchi waliojiandikisha kuweza kupiga kura kuchagua viongozi ambao ni chaguo lao.

Vituo vya wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi kamili jioni. Tukio hili la kupiga kura Novemba 27, 2024 halitajirudia tena hadi mwaka 2029 utakapoitishwa uchaguzi mwingine wa serikali za mitaa. Nikusihi mwananchi mwenzangu usipange kukosa kupiga kura kwani kura yako ndiyo maendeleo ya mtaa, kitongoji na kijiji chako. Kazi ni kwako.

Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

# MSCL sasa kuitwa TASHICO




**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

KAMPUNI ya Huduma za Meli (MSCL) imefanya mabadiliko ya jina la kampuni hiyo ambapo kwa sasa inaitwa Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) ikiwa ni sehemu ya kuongeza wigo katika huduma za usafiri wa majini.

Akizungumza kwenye hafla ya uzinduzi wa jina hilo jipya na nembo mpya ya kampuni hiyo uliofanyika jana katika Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza Mkurugenzi Mtendaji wa TASHICO, Eric Hamissi, alisema mabadiliko hayo ni sehemu ya kupanua wigo wa utoaji huduma sanjari na kujikita katika upanuzi wa biashara kwenye maeneo ya Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi.

Alisema lengo ni kuwa na meli nyingi zikiwemo za kubeba mizigo huku akieleza matarajio ya kuwa na meli katika Bahari ya Hindi.

"Tunatarajia kuwa na meli zisizopungua nne katika Bahari ya Hindi ifikapo mwaka 2030 lengo ni kuendeleza sekta hii ya uchukuzi ili iweze kuleta tija kwenye Taifa", alisema.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile ameielekeza menejimenti ya TASHICO kuongeza ubunifu katika eneo la huduma kwa wateja hususani kwa huduma za abiria na mizigo.

Pia aliwaasa kusimamia kwa karibu wakandarasi wa miradi yote inayotekelezwa kwenye ukarabati na ujenzi wa meli ikamilike kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu Serikali imetoa Sh. trilioni 1.2 kwa ajili ya kuboresha miradi ya meli kwenye Maziwa Makuu.

Awali akitoa salamu kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, Katibu Tawala wa mkoa huo Elikana Balandya, alisema miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwa imara inasaidia kuboresha uchumi wa wananchi hivyo akishukuru Serikali kwanamna inavyoendelea kuboresha sekta ya uchukuzi.



# Nguchiro: Mnyama mdogo jasiri wa kupambana na viumbe hatari



**NGUCHIRO** ni mnyama mdogo wa porini anayejulikana kwa jina la Kiingereza mongoose. Wanyama hawa wanapatikana Afrika, Asia, na baadhi ya sehemu za Ulaya, wakiwa na sifa mbalimbali za kipekee. Tabia zao zinavutia kutokana na uwezo wao wa kuishi katika mazingira tofauti, tabia za kijamii, na mbinu za kujilinda. Hapa ni maelezo ya kina kuhusu nguchiro:

## MUONEKANO WA NGUCHIRO

Nguchiro ni mnyama mdogo, mwenye mwili mrefu na mnyoofu, miguu mifupi, na mkia mrefu. Ngozi ya nguchiro kwa kawaida ni kahawia, kijivu au yenye mistari, kutegemea aina ya nguchiro.

Wana meno makali yanayofaa kula nyama, lakini pia wanaweza kula mimea na matunda.

## MAKAZI NA MAZINGIRA

Nguchiro hupatikana kwenye maeneo mbalimbali, kutoka savana za Afrika, misitu ya tropiki, hadi kwenye maeneo yenye ukame kama nyika.

Wanapenda kuishi karibu na miamba, mashimo, au vichaka vinavyotoa usalama kutoka kwa wanyama wakubwa na wanyama wawindaji.

## LISHE

Nguchiro ni wanyama walaji mchanganyiko, nyama na mimea (omnivores). Lishe yao inajumuisha nyama ambapo hula wadudu, mijusi, nyoka, ndege wachanga, na mamalia wadogo.

Kwa upande wa mimea, nguchiro hupendelea kula matunda, mbegu, na mizizi.

## TABIA ZA KIJAMII

Baadhi ya spishi za nguchiro huishi kwa makundi makubwa yanayojulikana kama "clans," ambapo ushirikiano na msaada wa kijamii huwa ni muhimu kwao.

Katika makundi haya, nguchiro mmoja hubaki kuwa mlinzi, huku wengine wakitafuta chakula. Wana mfumo wa mawasiliano wa sauti kuonya wenzao kuhusu hatari.

Spishi nyingine ni za upweke, na huishi peke yao isipokuwa wakati wa nguchiro jike anapopata joto na kuhitaji kupandwa pamoja na kulea watoto ambapo mara nyingi hushirikiana.

## UZAZI NA MALEZI

Nguchiro wanao uwezo wa kuzaa mara kadhaa kwa mwaka, kutegemea spishi na mazingira wanayoishi.

Wanazaa watoto wachache, kawaida wawili hadi wanne. Nguchiro hubeba mimba kati ya siku 42 na 105. Wazazi wote, na mara nyingine kundi zima, hushirikiana katika kuwalea watoto wachanga kwa kuwalinda na kuwapa chakula.

## TABIA ZA KUJILINDA

Nguchiro wana mwitikio wa haraka na mbinu nzuri za kujihami dhidi ya wanyama hatari, kama nyoka wenye sumu. Ni wanyama wadogo wanaojulikana kwa ujasiri mkubwa, hata wakikabiliana na wanyama wakubwa zaidi yao.

Nguchiro anaweza kujifanya amejeruhiwa ili kuvuruga mawindo au mnyama adui apoteze mwelekeo.

## MCHANGO WA NGUCHIRO KWENYE MAZINGIRA

Nguchiro husaidia kudhibiti idadi ya wadudu na wanyama wengine wadogo, jambo linalosaidia kuleta uwiano katika mfumo wa ikolojia. Wanajulikana pia kwa kudhibiti nyoka wenye sumu, hivyo kusaidia kuwalinda watu waishio karibu nao.

## CHANGAMOTO NA VITISHO

Nguchiro huwindwa na wanyama wakubwa kama tai, fisi, na simba. Kwa upande wa binadamu nguchiro hufanya uharibifu wa makazi yao, uwindaji, na sumu inayowekwa kudhibiti wadudu wa shambani huathiri idadi yao.

Kwa upande wa magonjwa, nguchiro wanaweza pia kuathiriwa na magonjwa kama kichaa cha mbwa.

## KINACHOMSAIDIA NGUCHIRO KULA NYOKA

Nguchiro wana umaarufu wa kipekee kwa uwezo wao wa kushambulia na kula nyoka wenye sumu kama vile koboko, kwa kuwa wana kasi na ujanja wa kuepuka mashambulizi ya nyoka.

Uwezo huu unatokana na mchanganyiko wa tabia, maumbile, na fiziolojia.

Moja ya kitu kinachomsaidia nguchiro kupambana na nyoka ni kuwa ana kinga ya kibaiolojia dhidi ya sumu. Nguchiro ana mwili wenye protini maalumu zinazozuia sumu ya nyoka kuathiri seli zake. Protini hizi zinabadilisha jinsi sumu inavyoshikamana na seli za mwili, hivyo kuzuia madhara.

Utafiti umeonyesha kuwa mnyama huyu ana protini inayojulikana kama acetylcholine receptor iliyobadilishwa, ambayo sumu nyingi za nyoka (kama zile za familia ya elapids, wakiwemo koboko na nyoka wa aina ya mamba) hushindwa kushambulia.

Pili, nguchiro ana ngozi nene na uwezo wa kuepuka kugongwa sana na nyoka. Ngozi ya nguchiro ni nene na yenye kunyumbulika, hivyo kupunguza uwezekano wa meno ya nyoka kupenya kwa urahisi hadi kwenye mishipa ya damu.

Hata pale anapogongwa, kiwango cha sumu kinachoingia mwilini huwa kidogo sana, hivyo mwili wake unaweza kushughulikia sumu hiyo bila madhara makubwa.

Kingine kinachomsaidia nguchiro katika mapambano yake na nyoka ni kasi na ujanja wa kupambana. Nguchiro ana kasi kubwa na ustadi wa hali ya juu wa kupigana. Wakati wa kukabiliana na nyoka, nguchiro hutumia mbinu za ujanja na kuruka mara kwa mara ili kuepuka shambulio la nyoka.

Ana uwezo wa kumchosha nyoka kwa kumshambulia mara kwa mara, hadi pale anapopata fursa ya kumuangusha.

Nguchiro pia ni mstahimilivu wa asili kwa maana ya kwamba hata kama nguchiro anaumwa na nyoka mwenye sumu kali, mara nyingi anaweza kuhimili athari za muda mfupi za sumu hiyo. Mwili wake unaweza kupunguza madhara hayo, na baada ya muda mfupi, anaweza kupona na kuendelea kula windo lake.


Nguchiro ana maarifa ya asili ya kushambulia nyoka kwa sehemu hatarishi kama kichwa au shingo, jambo linalompa nafasi ya kuwadhibiti nyoka kabla ya kushambuliwa vibaya.

Nguchiro si mtegemezi wa nyoka pekee kwa chakula. Lishe yake yenye virutubisho mbalimbali, kama wadudu na matunda, husaidia mwili wake kuwa na nguvu na kinga bora, hivyo kustahimili changamoto za mazingira, zikiwemo sumu za nyoka.

Kwa sababu hizi, nguchiro amekuwa mmoja wa wanyama wachache wenye uwezo wa kushinda vita dhidi ya nyoka wenye sumu na kuendelea kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa ikolojia kwa kudhibiti idadi ya nyoka hatari.

# Maaskofu wakataa mchango wa Ruto

## ● Wasema majukwaa ya Kanisa yasitumike kujinufaisha kisiasa



**NAIROBI, Kenya**

JIMBO Kuu la Kanisa Katoliki Nairobi, limesisitiza kujitolea kwake kuzingatia sera ya Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki nchini Kenya (KCCB) kuhusu michango ya kisiasa kanisani.

Novemba 17, mwsaka huu, Jimbo Kuu lilitangaza kukataliwa kwa michango kadhaa iliyotolewa katika Kanisa Katoliki la Soweto, kwa mujibu wa maagizo ya KCCB na Muswada wa Kuchangisha Fedha za Umma wa 2024.

Rais William Ruto alichangia Sh. milioni mbili kwa ujenzi wa nyumba ya Padri na kutoa ahadi ya Sh. milioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa ziada na mchango wa mabasi ya parokia.

KCCB, katika taarifa yake iliyotolewa Novemba, 14, mwaka huu na kusomwa katika makanisa yote ndani ya Jimbo Kuu Jumapili ya Novemba 17, mwaka huu, ilisisitiza umuhimu wa kuhifadhi uhuru na utakatifu wa Kanisa pamoja na masuala ya kimaadili yanayozunguka michango ya kisiasa.

Akizungumza kwa niaba ya Jimbo Kuu Askofu Mkuu Philip A. Anyolo, alisisitiza umuhimu wa majukwaa ya Kanisa kutotumiwa kujinufaisha kisiasa.

BBC

# Gari laparamia umati wa watu nje ya shule

**BEIJING, China**

GARI limeparamia umati wa watu nje ya shule ya msingi katika Mkoa wa Hunan Kusini mwa China na kusababisha majeruhi kadhaa.

Bado hakuna maelezo juu ya watu wangapi wamejeruhiwa, lakini vyombo vya habari vya serikali vinasema wanafunzi kadhaa na watu wazima, wamejeruhiwa na wako hospitalini.

Dereva wa gari hilo alikamatwa na wazazi na maafisa wa usalama wa shule na kukabidhiwa kwa polisi.

"Makumi ya watu waligongwa, baadhi yao vibaya, lakini gari la kubeba wagonjwa lilikuja haraka sana," asema mmoja wa wazazi wa wanafunzi hao, Zhu.

Shule hiyo imetambuliwa kuwa ni ya Msingi ya Yong'an katika Wilaya ya Dingcheng mkoani Hunan.

Video kutoka eneo la tukio iliyotumwa kwenye mtandao wa WeChat, inaonesha baadhi ya watoto wakiwa wamelala chini, huku wengine wakiwa wamebeba mabegi ya shule, wakikimbia kwa hofu.

Video nyingine iliyochukuliwa baada ya tukio hilo inaonyesha mtembea kwa miguu mwenye hasira akiigonga gari hiyo kwa koleo la kuondolea theluji wakati dereva akiwa bado ndani.

Kisha dereva huyo anaonekana akitoka upande wa pili wa gari hilo na kuzungukwa na watu ambao walianza kumpiga kwa fimbo.

Hili ni shambulio la tatu kwa umati wa watu nchini China katika wiki moja na limezua wasiwasi juu ya usalama wa umma.

BBC.

# Trump kutumia Jeshi kuhamisha wahamiaji



**WASHINGTON, Marekani**

RAIS Mteule Donald Trump amethibitisha kwenye mtandao wake wa kijamii kuwa anapanga kutumia Jeshi la Marekani kutekeleza operesheni ya kuwafukuza wahamiaji wasio na vibali nchini Marekani.

Siku ya Jumatatu, alichapisha kwenye mtandao wa "TRUTH!!!" akijibu maoni ya mhafidhina ambaye aliandika kwamba Trump atatangaza hali ya dharura ya kitaifa na kutumia jeshi kuongoza mpango wa kuwahamisha watu wengi.

Katika kampeni, Trump aliahidi mara kwa mara kutumia Walinzi wa Kitaifa kuwasaidia maafisa wa Uhamiaji na Forodha (ICE), ili kutekeleza jukumu hilo.

Kauli ya hivi punde ya Trump inakuja huku kukiwa na maswali kuhusu jinsi atakavyotimiza ahadi yake ya kuwafurusha watu wengi katika historia ya Marekani.

Alisema ataanza kuwahamisha siku yake ya kwanza ofisini, ambayo itakuwa Januari 20, mwakani.

Kauli ya Trump aliichapisha kwenye mtandao wake wa Truth mapema Jumatatu huku akiendelea kutangaza uteuzi katika nyadhifa muhimu katika utawala wake.

BBC.

# Misaada ya UN kwa Gaza yaporwa kwa bunduki

**GAZA, Palestina**

MSAFARA wa malori 109 ya misaada ya Umoja wa Mataifa (UN) yaliyokuwa yamebeba chakula yaliporwa kwa nguvu huko Gaza siku ya Jumamosi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (Unrwa), limesema.

Malori tisini na saba kati ya hayo madereva wake walilazimishwa kwa mtutu wa bunduki kushusha misaada hiyo baada ya kupita katika kivuko cha Kerem Shalom kinachodhibitiwa na Israel, Kusini mwa Gaza.

Walioshuhudia walisema msafara huo ulishambuliwa na watu waliojifunika nyuso zao na kurusha maguruneti.

Mkuu wa Unrwa, Philippe Lazzarini, hakuwatambua wahusika, lakini anasema kuporomoka kwa utulivu huko Gaza, kunamaanisha kuwa kuna mazingira yasiyowezekana kufanya kazi.

Bila uingiliaji kati wa haraka, uhaba mkubwa wa chakula unatarajiwa kuwa mbaya zaidi kwa watu milioni mbili ambao hutegemea misaada ya kibinadamu, kwa mujibu wa Unrwa.

Tathmini iliyoungwa mkono na UN ilionya mapema mwezi huu kwamba kuna "uwezekano mkubwa kwamba balaa la njaa linajongea katika maeneo ya Kaskazini mwa Ukanda wa Gaza."

Uporaji wa Jumamosi uliripotiwa kwa mara ya kwanza na Shirika la Habari la Reuters, ambalo lilimnukuu afisa wa Unrwa huko Gaza. BBC.

# Urusi yatoa msimamo makombora ya U.S. kwa Ukraine

**MOSCOW, Urusi**

RAIS Joe Biden aliidhinisha matumizi ya makombora kushambulia shabaha ndani ya Urusi katika mabadiliko makubwa ya sera ya Marekani miezi miwili kabla ya hajaondoka Ikulu ya Marekani.

Haijabainika iwapo mrithi wake, Rais Mteule Donald Trump, alishauriwa au iwapo atashikilia uamuzi huo, baada ya kuahidi kumaliza vita vya Urusi na Ukraine.

Ukraine imekuwa ikitumia makombora ya Marekani yenye uwezo wa kufika hadi kilomita 300 (maili 190) - pamoja na makombora ya Ufaransa na Uingereza ya Storm Shadow ya masafa marefu, lakini washirika hao wa Magharibi waliizuia Kyiv kushambulia ndani ya Urusi kwa makombora hayo.


Uamuzi wa Biden wa kuondoa kikwazo hicho kwa upande wa Marekani, umekuja wakati ambao vita hivyo vinaingia siku yake ya 1,000 jana.

Urusi ilifanya uvamizi mkubwa nchini Ukraine kuanzia Februari 24, mwaka 2022.

BBC.



# Buriani King Kiki, Mzee wa 'Kitambaa cheupe'



**Na Hamid Yassin**

MEDANI ya muziki wa dansi mwishoni mwa wiki iliyopita ilipata pigo kubwa baada ya kuondokewa na mwanamuziki mkongwe na nguli, Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki baada ya kuugua kwa muda mrefu.

King Kiki ni jina kubwa hasa kwa 'vijana wa zamani' waliokuwa wanazi wa muziki wa dansi, alitikisa vilivyo tangu alipoingia nchini mara ya kwanza mwezi Juni mwaka 1970 na kujiunga na bendi iliyokuwa inaongozwa na marehemu Ndala Kasheba ya Fouvette Muzica.

Baada ya kukaa hapa nchini kwa miezi sita, King Kiki, Kasheba na wanamuziki wengine waliounda bendi hiyo ya Fouvette waliondoka nchini kurejea kwao Congo DR wakati huo ikijulikana kama Zaire kupitia nchi za Burundi na Uganda.

Marehemu King alirejea tena nchini miaka saba baadaye, yaani mwaka 1977 na kujiunga na kundi la Maquizi du Zaire lililokuwa linaongozwa na mwanamuziki, Mwema Mujanga 'Mzee wa Chekecha mpaka chini'.

King Kiki hakukaa sana Maquize, kwani Mzee Hugo Kisima aliyekuwa anamiliki bendi ya Ochestre Safari Sound (OSS) alimchukua na kwenda kuimarisha bendi kiasi kuwa wapinzani wakubwa wa Maquzi kwenye viunga vya muziki wa dansi hapa nchini.

Kabla ya kwenda OSS pale Maqule aliibuka na mtindo wa 'Kamanyola', ambapo akizungumza enzi za uhai wake, King Kiki alisema kuwa, Kamanyola ni mji kule Congo DR, sasa yeye aliongeza maneno 'Bila Jasho' kwa maana kuwa mchezaji wa muziki huo atacheza taratibu kwa raha zake. Alitunga mtindo huo baada ya kujiunga na bendi hiyo mwaka 1977.

King Kiki alizaliwa Januari Mosi mwaka 1947 na alianza kuimba mwaka 1962 baada ya kuacha masomo akiwa sekondari kwa sababu muziki ulimwiingia katika damu.

Alijiunga na Bendi ya Fouvette kabla ya kubadilishwa jina na kuitwa Safari Nkoi ambayo waliingia nayo Tanzania chini ya Fred Ndala Kasheba miaka ya 1970.

Mwaka 1983 alianzisha bendi yake ya King Kiki Double O na mtindo wa Embalasasa Shika Breki.

Bendi hiyo ilikufa kutokana na uchakavu wa vyombo, baadaye akajiunga kwa muda Bendi ya Sambuluma na Nguza lakini mwaka 1994 akiwa na marehemu Ndala Kasheba wakaanzisha Bendi ya Zaita Musica.

"Mwaka 2003 nikiwa na Ndala huyohuyo tukaanzisha Bendi ya Wazee Sugu La Capital. Bahati mbaya mwenzangu Kasheba akafariki dunia mwaka mmoja baadaye, yaani 2004, lakini mpaka sasa nina bendi mbili, moja ipo Mwanza," aliongea King Kiki enzi za uhai wake.

Akizungumzia mafanikio yake ya kimuziki enzi za uhai wake, Kiki alisema ana historia ndefu, lakini kwa kifupi alisema anamshukuru Mungu kwani ana mafanikio ya kawaida, ikiwemo kumiliki nyumba Temeke Wailes (Dar) kubahatika watoto tisa , lakini wawili walishafariki dunia.

King Kiki ameacha mke Mtanzania na bendi mbili. Pia aliwahi kuzuru Uingereza baada ya kupata mwaliko mwaka 2011, pia alikwenda Marekani kufuatia kualikwa katika sherehe ya miaka hamsini ya uhuru wa Congo DR.

Marehemu King Kiki amefariki akiwa na Uraia wa Tanzania alioupata mwaka 1997 baada ya kuukana ule wa asili yake ya Congo DR.

Akielezea sababu za kuamua kuishi Tanzania na kuchukua uraia, King Kiki alisema enzi za uhai wake ni kutokana na ukarimu wa Watanzania.



Alisema alipofika hapa mara ya kwanza mwaka 1970, aliona watu ni wakarimu sana, akaamua kurudi mwaka 1977 na kuishi hapa.

Kiki alitunga nyimbo nyingi, hamsini kwenye Bendi ya Marquis na ishirini Safari Sound. Kuna wakati alikuwa na uwezo ndani ya wiki mbili kutunga nyimbo ishirini.

Baadhi ya nyimbo zilizotikisa ni 'Kyembe', 'Safari yetu Mbeya', 'Nasema sina ndugu', 'Msimamo wa Nyerere', 'Noele' (Krismas), 'Haruna Kaka' na iliyotamba na kuendelea kupigwa sana hadi leo ni ule wa 'Kitambaa Cheupe'.

Mbali ya kuimba, Kiki alisema enzi za uhai wake kuwa alikuwa anaweza kupiga magitaa yote lakini alikuwa anapendelea kuimba kwani hata Waswahili walisema 'kila ndege na mti wake'. Katika watoto wake, Veronica Kikumbi amefuata nyayo zake, alikuwa anaimba naye, hata ule wimbo wa 'Fungua Njia' alirekodi naye.

Juu ya kuporomoka kwa muziki wa dansi kwenye miaka ya hivi karibuni, Kiki alisema kama angepatikana mdhamini angerekodi upya nyimbo zilizovuma na zikatangazwa, kukafanyika onesho na maajabu makubwa yangeonekana.

Buriani King Kiki, Mzee wa 'Kitambaa Cheupe'.

**Kwa maoni na ushauri, 0713 315 966 ama 0618 179 727.**

# Fred Gordon Kiluswa; Nyota angavu iliyozima mapema

**Na Mwandishi Maalumu**

ILIKUWA Oktoba 10 akiwa hospitalini, Fredy Gordon Kiluswa aliposti hii katika mtandao wake wa kijamii wa Facebook; "Almighty and everlasting God, I acknowledge your blessing in the recovery of my health, and return to you my most hearty thanks for it.'

Fred Gordon Kiluswa, jina litakalokumbukwa kwa muda mrefu katika tasnia ya filamu nchini, ametuacha ghafla Novemba 16, akiwa katika matibabu ya ugonjwa wa moyo pale kwenye Hosptali ya Mlogaznzila.

Kiluswa ambaye uigizaji wake unatokana na kupitia shule zinazofundisha sinema kama Bagamoyo na Udom, alikuwa zaidi ya muigizaji; alikuwa msanii wa kweli ambaye aliweza kuigiza kila hisia, kutoka kwa furaha hadi huzuni, kwa njia ambayo iliwagusa mioyo ya watazamaji.

Kwa sasa alikuwa anatamba na tamthilia inayoendelea katika Televisheni ya Azam ya 'Mzani wa Mapenzi'.

Uigizaji wake ulikuwa wa kipekee. Alifanikiwa kuingia katika kila nafasi aliyoigiza, na kuwafanya watazamaji wahisi kama wamekuwa sehemu ya hadithi hiyo. Alikuwa na uwezo wa kuonesha hisia zake kwa njia ya wazi na ya kweli, na hii ndiyo ilivyomfanya kuwa mpendwa na kuheshimiwa na wengi.

Katika moja ya mahojiano na televisheni za Tanzania alisema alianza kuigiza kwa kazi moja ya Johari ambapo alikuwa mhusika mkuu akiwa na Uwoya.

Anasema kabla ya kuingia katika kuigiza awali alitaka kuwa mwanasheria lakini baada ya kumaliza sekondari alimua kwenda kujifunza kuongoza sinema katika Chuo cha sanaa Bagamoyo (Tasuba) kabla ya kwenda Udom kukamilisha zaidi uongozaji na utengenezaji wa sinema.

Kifo chake ni pigo kubwa kwa tasnia ya filamu nchini kwani itakosa sana mchango wake katika kuimarisha na kukuza sanaa hii. Alibaki kuwa miongoni mwa vipaji vichache vilivyokuwa vikipiga hatua kubwa katika uwanja huu kuelekea kuwa mwongoza sinema mahiri kama mwenyewe alivyotaka.

Aidha, mwamba huyu alishatwaa tuzo mwaka 2023/2024 na na akiwa na marafiki elfu 4.9 kwenye mtandao wake wa Instgram, amekuwa akitamba katika filamu na tamthilia mbalimbali ikiwemo tamthilia ya 'Mizani ya Mapenzi' inayoonyeshwa katika channel ya Sinema Zetu ya Azam TV na 'Lawama'.

Watu waliokuwa wanatoa maoni yao katika mitandao ya kijamii wamekuwa wakimwelewa sana hayati Fredy.

Kufuatia kifo hicho, mwongozaji msaidizi wa tamthilia ya 'Mizani ya Mapenzi' Alex Mgeta maarufu kama 'Ngosha' amesema mpendwa wao alikuwa akisumbuliwa na tatizo la moyo.



Ngosha ambaye ni mwongozaji msaidizi wa tamthilia hiyo ya 'Mizani ya Mapenzi' aliyokuwa akiigiza Fredy amesema kuwa marehemu aligundulika kuwa na tatizo hilo miezi miwili iliyopita.

"Alikuwa na shida ya moyo, alikuwa anaumwa muda kama wa miezi miwili nyuma alitibiwa akajisikia nafuu akarudi uraiani, akaanza kutumia dawa kama kawaida baadaye ikafikia hiyo hali ambayo siyo nzuri ndiyo ikamletea matokeo haya lakini awali alikuwa afanyiwe oparesheni wataalamu wakaona wampe kwanza dawa akaendelea vizuri kabisa baadaye gafla hali ikabadilika."

Ngosha aliongeza kuwa, mara ya mwisho presha ya Fredy ilikuwa juu sana kwa hiyo wakati ipo juu wataalamu walisubiri ishuke ili waendelee kutoa matibabu, ikasubiriwa ishuke wakafanya wanaloweza kufanya lakini haikuleta matokeo ambayo waliyatarajia.

Baba wa marehemu mwigizaji Fredy Kiluswa, Nahum Kiluswa, akiongelea kifo cha mwanaye ametanabahisha kuwa, kwa mara ya kwanza kijana wake alipata maradhi ya moyo akiwa safarini mwezi mmoja uliopita.

Kiluswa amesema kuwa Novemba 16, 2024, marehemu alipozidiwa alikimbizwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na kuwekwa kwenye chumba cha uangalizi maalumu.

"Hali yake ilikuwa mbaya, alikuwa akipumua kwa shida, huku presha yake ikiwa juu na haikushuka kwa muda mrefu".

Ameongeza kuwa marehemu hakuwa na historia ya magonjwa hayo hata alipokuwa mtoto.

Akizungmzia usanii wa mwanaye, Mzee Nahum amesema anakumbuka mambo mengi na alianza kupenda fani hiyo tangu akiwa mdogo na alipomaliza kidato cha nne alimuuliza anachotaka akamjibu alipendelea sanaa, ndipo alipompeleka Chuo cha Tasuba pale Bagamoyo.

Fredy Kiluswa, aliyezaliwa mwaka 1992, ameacha mke na watoto wawili. Mwili wake ulitarajiwa kuagwa jana Jumanne, Novemba 19, 2024, katika viwanja vya Leaders Club kisha kuzikwa katika makaburi ya Kinondoni.



# Je, Ramovic mrithi sahihi wa Gamondi Yanga?

Na Hamid Yassin

KLABU ya Yanga imemtambulicha Saed Ramovic raia wa Ujerumani kuwa kocha mpya wa timu hiyo baada ya kuachana na aliyekuwa kocha wao, Miguel Gamondi rai wa Argentina.

Sead Ramovic alikuwa akifundisha katika klabu ya TS Galaxy inayoshiriki ligi kuu nchini Afrika Kusini ambayo alijiunga nayo mwezi Oktoba mwaka 2021 akitokea FK Novi Pazar ya Serbia.

Ramovic mwenye umri wa miaka 45 alishawahi kufundisha katika vilabu vya VFL Wolfsburg na Borrusia M' Gladbach vyote vya Ujerumani katika miaka ya 2000 .

Ramovic, aliyepachikwa jina la 'Chuma cha Kijerumani'na Wanayanga, anachukua nafasi hiyo moto baada ya kocha aliyepita Gamondi, kufutwa kazi kufuatia vipigo viwili katika ligi ya Tanzania.

Kwa sasa, Yanga inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi, ikizidiwa alama moja na Simba SC ambao wako kileleni wakiwa na pointi 25.

Katika juhudi za kushindania makombe yote msimu huu, Yanga imeamua kumleta Ramovic, kocha aliyethibitisha uwezo wake akiwa na TS Galaxy, maarufu kama 'Rockets'.

Raia huyo wa Ujerumani, ambaye ana leseni ya juu kabisa ya ukocha (UEFA Pro License), alitumikia TS Galaxy kwa misimu mitatu tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka 2021 kwa mkataba wa miaka mitatu.

Ramovic aligeuza Galaxy kuwa moja ya timu za kuvutia zaidi nchini Afrika Kusini kwa mtindo wake wa soka lenye kasi na presha kubwa. Mashabiki wa Yanga sasa wanasubiri kuona kama ataweza kuleta mafanikio yanayotarajiwa ndani ya klabu hiyo kongwe ya Tanzania.







### KLABU NA MAKOCHA ALIOFANYA KAZI NAO

Ramovic alikuwa kocha mkuu wa TS Galaxy FC kuanzia Oktoba 1, mwaka 2021 hadi Novemba 2024, kabla ya hapo alikuwa kocha msaidizi wa timu ya FK Novi Pazar ya Serbia kuanzia Desemba 31 mwaka 2020 hadi Oktoba 1, 2021.

Pia alikuwa kocha msaidizi wa makocha wafuatao, Vladica Petrovic (mechi 32), Kenan Kolasinac (mechi 25), Zoran Maric (mechi 24), Nesko Milovanovic (mechi 16), Mladen Dodic (mechi 16), Marjan Zivkovic (mechi 16)na Darko Tesovic (mechi 13).

Makocha wengine wenye majina yao Ramovic amefanya kazi chini yao ni, Izet Ljajic (mechi 9), Slavko Matic (mechi 8), Nebojsa Vucicevic (mechi 7), Stevan Mojsilovic (mechi 7), Petar Kurcubic (mechi 7), Zoran Govedarica (mechi 6), Radmilo Ivancevic (mechi 6) na Radoslav Batak (mechi 5).

### RAMOVIC AKIWA MCHEZAJI

Ramoviv alikuwa akicheza nafasi ya kipa enzi zake.Alicheza soka kwa misimu 14 tangu Februari mwaka 2001 akizitumikia timu 11 tofauti, zikiwamo za Borusia M'gladbach na VfL Wolfsburg za Ujerumani, mara nyingi akihama kutoka klabu moja kwenda nyingine kwa uhamisho huru au kwa mkopo hadi alipostaafu kucheza soka Mei 21, 2014 akiwa na klabu ya Stromsgodset IF ya Norway.

Klabu nyingine alizochezea enzi zake katika mataifa kama Ujerumani, Uturuki, Norway, Denmark na Serbia ni Vendsyssel FF, Lillestrom SK, FK Novi Pazar, Metalurg Zaporizhya, Sivasspor, Tromso IL na Kickers Offenbach.

### TIMU YA TAIFA

Ramovic aliitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Bosnia & Herzegovina kwa mara ya kwanza mwaka 2004. Licha ya kuitwa katika kikosi hicho mara kadhaa, hakuwahi kucheza mechi hata moja ya kimataifa.

### MUUMINI WA NIDHAMU

Kubomoka kwa nidhamu ya wachezaji wa Yanga, wengi watawalaumu nyota wao, lakini kuna hawa wapambe ambao sasa wanaitwa 'chawa'. Uongozi wa klabu hiyo ni lazima uwatazame chawa hawa kwa jicho la ukali kwani wana ushawishi mbaya kwa wachezaji.

Kocha Ramovic amejipambanua toka timu alitoka kwamba yeye ni muumini wa nidhamu kwa wachezaji wake wakiwa ndani na nje ya mchezo.

Ameshaweka wazi kwamba, marufuku kwa wachezaji kulewa wala kuendekeza starehe nyingine kama kwenda klabu nyakati za kambi au mashindano.

Wachezaji kadhaa wa Yanga wakiwemo wale nyota wanaolalamikiwa kuwa, viwango vyao vimeporomoka wamekuwa wakionekana kwenye kumbi za starehe wakinywa pombe na kuvuta shisha bila kificho chochote kile!

Hapa wale viongozi wanaowaendekeza hao wachezaji nyota watamtafuta ubaya kocha Ramovic kwani hakubaliani asilani na tabia hizo.

Kocha aliyetimuliwa, Gamondi hakuwa na nongwa kwa wachezaji wake 'kujirusha' huku wakati mwingine akijumuika nao kula 'bata' kwenye viunga mbalimbali vya burudani!

Hawa 'chawa' wanaowaharibu wachezaji, ukizunguka usiku unakutana nao wako na wachezaji wao, kukicha utawaona wako na viongozi wao, likishaibuka balaa kama hili la Gamondi, haraka wanakaa upande wa viongozi.

Kundi hili ni hatarishi zaidi, linajua kuunganisha watu na kisha kukaa pembeni wanasubiri anguko ili kisha wauwashe moto. Nani anatakiwa kuokoa jahazi? Ni viongozi wenyewe kwa kuwaambia ukweli wachezaji wao kwamba wanaokaa nao na kufanya nao starehe ndio haohao watasambaza mambo yao endapo watakosa kujitambua kufanya mambo yao bila ya weledi.

Wachezaji wa Yanga waache dharau na kuishi kwa mazoea, wanatakiwa kutambua ligi ni ngumu na kila timu inautaka ubingwa, watani wao simba wamebadilika, wamefanya usajili mkubwa na kiufupi kila timu imejipanga kwa hesabu zake, hivyo haitakuwa rahisi kwao kutetea ubingwa endapo wataendelea kujiona kama wao ndio bora kuliko wengine.

Tunawajua wachezaji wanaodekezwa, wakiona kocha wao mpya, Ramovic anawabana katika starehe zao walizoea, watamwanzishia mizengwe kocha huyo ikiwemo kutojituma uwanjani ili kumkomoa.

Katika hili wanaoweza kuliweka sawa ni viongozi wa Yanga chini ya Rais wao, Eng. Hersi Saidi, kinyume na hapo wataendelea kufukuza makocha kila msimu hata kama timu yao itaendelea kufanya vizuri na kutwaa mataji!

**Kwa maoni na ushauri; 0713 315966 ama 0618 179 727.**

# Wachezaji hawa ni uti wa mgongo Simba

**Na Hamid Yassin**

UNAPOTAJA ubora wa Simba kwa sasa kuna wachezaji walioshikilia uti wa mgongo wa Simba hususani kwenye mbinu na mifumo yote ya kocha, Fadlu Davids tangu awasili kikosini hapo.

Kwenye michezo 10 iliyowaweka Simba kileleni ikiwa ndiyo timu yenye takwimu bora kuliko timu yeyote Ligi Kuu ya NBC mpaka sasa, kufanya kwao vema kunachangiwa na ubora wa baadhi ya wachezaji wao.

Ingawa kocha Fadlu ameshawatumia wachezaji wote wa ndani kwenye mechi za ligi ukimuondoa beki wa kulia, David Kameta 'Duchu, lakini kuna baadhi ya wachezaji ndiyo muhimili wa timu hiyo kwa sasa.

**JEAN AHOUA**

Simba ilikuwa inahangaika kupata mchezaji mwenye uwezo wa kuunda mashambulizi, kuyafanyia mwendelezo na kuwa mmaliziaji kwa wakati mmoja ili kutoonekana pengo la Clatous Chama ambaye kwa miaka bora yote ya Simba alikuwa mwiba hatari kwenye mifumo ya kila mwalimu aliyekuja viunga vya Msimbazi.

Jean Charles Ahoua amecheza michezo 9 kati ya 10 iliyocheza Simba, akifunga magoli matano pasi nne za usaidizi wa magoli na mashuti tisa yaliyolenga langoni huku nane yakienda fyongo.

Katika magoli hayo amefunga kwa penalti mara 2, amefunga magoli 4 ndani ya 18, goli moja nje ya yadi 18 za goli. Kipindi cha kwanza amefunga magoli mawili, kipindi cha pili amefunga magoli matatu; nazungumzia michezo 8 katika 10 ambayo mnyama Simba amecheza.

**DEBORAH FERNANDES MAVAMBO**

Tangu kuondoka kwa James Kotei, Greyson Fraga, Thadeo





Lwanga, Simba imekuwa ikihaha kuwa na namba sita asili ama mwenye sifa za kucheza kiungo cha chini na kuiziba safu ya ulinzi isifikiwe kirahisi lakini pia kuisukuma timu juu ipate urahisi wa kushambulia.

Mavambo amecheza michezo tisa 9 katika 10 ya Simba mpaka sasa, amefunga goli moja 1, hajatoa pasi za magoli (assist), amepiga mashuti matatu yaliyolenga lango huku matano yakitoka nje, ingawa anacheza kiungo mzuiaji, Mavambo hana kadi nyekundu wala njano!

Huyu ni kiungo wa kisasa (Modern Middlefield) anaweza kucheza kiungo cha chini na juu, anaweza kwenda kama 'box to box', anaweza kuvunja kama namba 8 ama ukihitaji viungo wawili wa ulinzi 'double pivot' Mavambo anamudu na atasambaza upendo bila shida.

**CHE MALONE PONDA**

Amecheza dakika 900 za michezo 10 ya ligi amefunga magoli mawili na ana kadi moja ya njano, ni



mchezaji aliyecheza michezo mingi na dakika nyingi kwenye kikosi cha Simba.

Ameruhusu magoli matatu machache kuliko timu yeyote ligi kuu amesaidia eneo lake golini kuondoka na 'clean-Sheets' 8 katika michezo 10, ukuta wake una nidhamu ya hali ya juu.

**MOUSSA CAMARA**

Kipa aliyesajiliwa msimu huu akitokea timu ya Holaya ya Guinea amekuwa sehemu ya muhimili muhimu wa klabu yake akiwa amesimama langoni katika michezo yote kumi ya Ligi Kuu timu yake iliyocheza.

Katika michezo hiyo kumi, Camara ameondoka na bila kufungwa katika mechi nane na ameruhusu nyavu zake kutikiswa mara mata tatu katika michezo miwili.

Ingawa alipata lawama kubwa kutoka kwa baadhi ya viongozi na wapenzi wa Simba kutokana na jinsi alivyofungwa hayo magoli matatu, lakini Camara anabaki kuwa nguzo muhimu kwa Simba na ana mchango mkubwa kwa mnyama kukaa pale kileleni hadi muda huu.

**KAPOMBE**

Huyu ni mchezaji mwandamizi pale Msimbazi, amecheza vema dakika nyingi msimu huu upande ule wa kulia ingawa kuna nyakati humpisha beki mpya, Kelvin Kijili kwenye kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi.

Kapombe pamoja na kuwa umri umesonga kiasi lakini bado amekuwa na mapafu ya mbwa, yaani anapanda na kushuka muda wote wa mchezo, anazuia kwa umakini sambamba na kushambulia kwa ufasaha.

Hadi wakati huu Ligi Kuu ikiwa imesimama kupisha mashindano ya kimataifa ya timu ya taifa na yale Klabu Bingwa na Shirikisho ya Afrika, Kapombe ameshafunga goli moja na kutengeneza mengine mawili kwa timu yake.

Na baada ya muda mrefu, kocha wa timu ya taifa, Hemed Selemani 'Morocco' amemrudisha kikosini kwenye mechi zilizosalia za Kombe la Mataifa ya Afrika za Ethiopia na Guinea ili atoe mchango wake kwenye azma ya kuipeleka Taifa Stars kwenye fainali za AFCON mwakani kule nchini Morocco.

**TSHABALALA**

Akiwa ndiye mchezaji wa muda mrefu zaidi ndani ya kikosi cha Simba hivi sasa, Mohamed Hussein 'Tshabalala' hachuji miaka nenda rudi moto wake ni ule ule pale Msimbazi!

Kwa sasa ndiye nahodha wa kikosi hicho akiwa amerithi mikoba ya John Bocco aliyetimikia timu ya JKT Tanzania.

Tshabalala amecheza karibu michezo yote ukiondoa ule wa mwisho kabla ya ligi haijasimama Simba iliocheza dhidi ya KMC na kushinda bao 4-0 ambapo alimpisha beki mpya wa kushoto



wa timu hiyo, Mbukinabe, Valentine Nouma.

Kwa msimu kadhaa Tshabalala amekuwa akiletewa mabeki wa ndani na nje ya nchi wa kumpa changamoto kwenye nafasi hiyo, lakini hakuna hata mmoja aliyemudu kumpeleka kukaa kwenye mbao ndefu!

Kama kawaida, msimu huu nao anaupiga mwingi hadi 'unamwagika'! Ameshafunga goli moja na kutoa pasi mbili za usaidizi wa magoli na kocha Fadlu humwambii kitu mbele ya nahodha wake huyu.

**HAMZA NA KAGOMA**

Hawa walianza msimu vizuri, lakini wakumbwa na majeraha yanayoendelea kuwaweka nje ya kikosi hadi sasa.

Pia kuna wachezaji kama Awesu Ally Awesu, Leonel Ateba, Steven Mukwala, Kibu Denis na Joshua Mutale hawa wamekuwa na uhakika wa namba na wana mchango wao msimu huu kwenye mafanikio ya Simba hadi sasa.

**Kwa maoni na ushauri; 0713 315966 ama 0618 179 727.**



Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Novemba 20-26, 2024 |

# Mbokani apigwa chini na mpenzi, kisa kustaafu soka!



**PARIS, Ufaransa**

MWANADADA Marlène Ntesa ameachana na nyota wa soka wa Congo, Dieumerci Mbokani kwa sababu anafikiri mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38 hatakuwa na pesa za kumtunza baada ya kustaafu kucheza soka.

Ntesa ametamka kwamba, hataki tena kuwa na uhusiano na Dieumerci kwa sababu anaamini hatakuwa na pesa za kutosha kukidhi mahitaji yake kama ilivyokuwa huko nyuma.

"Kila kitu kimekuwa kigumu kwake tangu siku alipoamua kustaafu kimataifa, nilimpenda kwa kumuonea huruma, na sasa ninahisi hatuwezi kuwa wanandoa tena labda awe mchezaji tena," amedai Ntesa.

# Morrison: Mpanzu atawatesa sana

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa zamani wa klabu za Yanga na Simba, Bernard Morrison ametamka kuwa, winga mpya wa timu ya Simba, Elia Mpanzu analijua soka na atazitesa sana timu zitakazokutana na Wekundu hao wa Msimbazi.

Morrison ametoa kauli hiyo wakati akijibu swali la mdua wa soka juu ya nyota huyo aliyetokea AS Vita, amebainisha kuwa, amemshuhudia Mpanzu akicheza wakati yeye alipokuwa anacheza soka kwenye timu ya AS Vita miaka kadhaa iliyopita.

Mghana huyo ambye yuko nje ya dimba kwa muda mrefu sasa kutokana na kuwa majeruhi amesema kuwa, kama Simba itamtumia vizuri Mpanzu anayemudu kucheza winga zote mbili samba na kucheza nyuma ya mshambulia, anaweza kuwapatia mafanikio makubwa kwenye michuano ya ndani na ya kimataifa.

Mpanzu ambaye alitambulishwa September Mwaka huu, hajaanza kuichezea timu hiyo kutokana na kutua baada ya kufungwa kwa usajili wa dirisha kubwa, huenda akaonekana uwanjani kwa mara ya kwanza Desemba 15 mwaka huu.

Baada ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kucheza mechi yeyote ya mashindano, Desemba 15 mwaka huu Simba itakapokuwa na mchezo wa Kombe la Shirikisho dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, Mpanzu anaweza kuonekana Uwanjani Endapo kocha Fadlu Davids atampa nafasi.

Kocha Simba, Fadlu Davids, amesema anafurahia namna wachezaji wake huyo anavyocheza na kwa sasa yeye pamoja na wenzake wa benchi la ufundi wanaangalia jinsi watakavyomtumia.

Akizungumzi timu yake kwa ujumla, Fadlu amepasha kuwa, anafurahishwa na jinsi wachezaji wake wanavyopambana, hata hivyo, bado kuna kitu anakitafuta kutoka kwenye kikosi chake lakini bado hajakipata.

"Bado kuna kitu nakitafuta na sijakipata, hili nalifanyia kazi kwa sababu kuna wakati tunakuwa katika ubora unaotakiwa, lakini baadaye tunashuka, mchezo mmoja tunakuwa na kasi tofauti, tunapanda na kushuka, hili ni tatizo, nadhani tukicheza kwa kasi kwa dakika zote 90, Simba itakuwa hatari sana," amedai kocha wa Simba Fadlu.



# Zahera amtoa Bacca Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

UBORA na nidhamu ya mchezo aliyonayo beki wa kati wa Yanga, Ibrahim Hamad 'Bacca' imetosha kumfanya kocha Mwinyi Zahera kumchomoa nyota huyo kikosini hapo huku akimwambia jambo la kufanya.

Zahera raia wa DR Congo aliyewahi kuifundisha Yanga ambaye sasa anahudumu kamMkurugenzi wa Ufundi wa timu ya Namungo ya Lindi, amesema Bacca anapoteza muda kucheza Ligi ya Tanzania kutokana na ubora alionao kwenye eneo analocheza.

Akizungumza mapema wiki hii, Zahera amesema Bacca ameonyesha uwezo mkubwa Ligi Kuu, hivyo sasa ni wakati wa kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania kwa sababu uwezo na sifa anazo na muda anaoupoteza yatamtokea kama ya Clement Mzize aliyepokea ofa nyingi, lakini hakupata nafasi ya kutoka.

"Kuwazuia wachezaji kwenda kujaribu maisha mengine nje ya timu wanazozichezea ni kuua ubora wa timu ya taifa, mfano mzuri ni kwetu Congo DR tuna timu nzuri kwa sababu tuna wachezaji wengi wazuri wanaocheza nje ya taifa letu na wamekuwa msaada mkubwa wa ujenzi wa timu yetu bora ya taifa."



# Morocco aipeleka Stars Morocco

## ● Msuva kama kawaida aibeba Tanzania
## ● Tiketi za Dk. Samia zimelipa, uwanja ulifurika

**Na Hamid Yassin**

TIMU ya taifa 'Taifa Stars' imefanikiwa kutinga fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara ya pili mfululizo na mara ya nne katika historia ya Tanzania baada ya kuifunga Guinea bao 1-0 pale Uwanja wa Mkapa 'Lupaso'.

Safarini hii Tanzania ilikuwa inaongozwa na benchi la ufundi la makocha wazalendo watupu kwa mara ya kwanza huku Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa amewalipia mashabiki wote waliofulika kwenye uwanja huo.

Stars ilianza kwa shambulizi la mapema la dakika ya kwanza tu, lakini kipa wa Guinea, Moussa Camara aliokoa mpira uliopigwa na nahodha Mbwana Samatta.

Stars ilirudi tena kwenye lango la Guinea dakika ya nne, lakini shuti la Feisal Salumu lilimbabatiza beki wao na kuwa kona tasa.

Dakika ya 9 Aishi Manura alifanya kazi ya ziada kuokoa mpira wa mshambuliaji wa Guinea Seydouba Cisse.

Naye Simon Msuva alikosa bao la wazi dakika moja baadaye baada ya kupiga shuti fyongo akiwa analitizama goli kufuatia pasi murua ya Feisal.

Stars iliendeleza mashambulizi mfululizo lakini umaliziaji mbaya na na kupiga krosi nyingi za juu ziliwagharimu kwani mabeki na wachezaji wengi wa Guinea ni warefu sana kuliko wale wa Taifa Stars.

Clementi Mzize alipoteza nafasi nyingine kwa Stars kupata bao la kuongoza katika dakika ya 33 ya mchezo baada ya kupiga kichwa mpira uliopata juu ya lango kufuatia shambulizi la kushtukiza la Stars.

Dakika ya 36 ya mchezo kocha Hemed Seleman' Morocco' alitaka kumwingiza Kibu Denis kuchukua nafasi ya Clementi Mzize, lakini mchezaji huyo akasema yupo fiti kuendelea na Kibu akarudi benchi kukaa.



Dakika ya 41 Stars ilinusurika kufungwa baada ya wachezaji wa Guinea kugongeana vema lakini shuti lililopigwa na Mohamed Camara liligonga 'Mtambaa panya' na kurudi uwanjani na kuokolewa.

Kipindi cha pili Stars ilianza na mabadiliko ya kumwingiza winga Kibu Denis kuchukua nafasi ya Mzize.

Kwa mara nyingine Msuva aliinyima Stars bao la kuongoza katika dakika ya 50 baada ya kuunganisha ovyo krosi ya Kibu akiwa hatua chache kutoka kwenye lango la Guinea.

Msuva alikosa bao la tatu katika mechi hii katika dakika ya 58 baada ya kupiga shuti lililopaa juu ya lango la Guinea kufuatia pasi ya nzuri ya Shomari Kapombe.

Baada ya kupoteza nafasi tatu za wazi, hatimaye Msuva katika dakika ya 60 aliifungia Stars bao la kuongoza kufuatia pasi maridhawa ya Mudathiri Yahya na kuwainua maelfu ya mashabiki waliojaa kwenye Uwanja wa Mkapa ambao walilipiwa kiingilio na Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan.